Jumamosi Aprili 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580903

www.ippmedia.com

MWANGA WA JA

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook hetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US






**Mama** asakwa kwa tuhuma kumzalisha binti yake kwa kitu chenye ncha kali

UKURASA 7



**BUSQUETS ANA NDOTO MESSI KUREJEA BARCELONA**

UKURASA 22

# Kinana: Demokrasia ianzie ndani ya CCM

• **Aahidi** kutenda haki. Aanika alivyoteta na Samia kabla ya uteuzi, aonya ukabila, ukanda, udini. Makamba, Wassira, Mrema, waliamsha... *Endelea ukurasa 2, 3 na 7*




Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana, akizungumza wakati akitoa shukrani kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa chama hicho, kwa kumchagua kwa kura nyingi kushika nafasi hiyo, jijini Dodoma jana. Watatu kushoto ni Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**SABABU ZA MANGULA KUNG'ATUKA UONGOZI**

MAKAMU Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula, amesema ameng'atuka...

**Mbaroni kwa tuhuma za kujitengenezea tukio ujambazi**

UKURASA 4

Meneja Matangazo wa kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), Angel Navuri (kushoto), akipokea Tuzo ya Super-Brand Afrika Mashariki, kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chandaria Industries, Darshan Chandaria, iliyotolewa kwa kampuni hiyo, katika hafla iliyofanyika jijini Nairobi, Kenya. **PICHA: MPIGAPICHA**




# Wizara hii kaa la moto, miaka 60 mawaziri 24

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YATANGAZA MAPAMBANO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu mstaafu Cleopa David Msuya (kushoto), akisalimiana na Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Mzee Yusufu Makamba, walipokutana kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vipaumbele vya Kinana umakamu mwenyekiti

**Epson Luhwago na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, jana alichaguliwa kwa kishindo kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho huku akitaja vipaumbele vitatu.

Kinana pia ameahidi utumishi uliotukuka na si utukufu uliotukuka.

Katika uchaguzi huo uliofanyika sambamba na Mkutano Mkuu Maalumu wa Taifa wa CCM katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini hapa, Kinana alipata kura 1875 sawa na asilimia 100.

Kinana alichaguliwa kushika nafasi hiyo baada ya aliyekuwa akishika nafasi hiyo, Philip Mangula, kuwasilisha barua ya kung'atuka. Mangula alitumikia nafasi hiyo kwa miaka 11 akipokea kijiti kutoka kwa Pius Msekwa.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Kinana alisema mambo ya muhimu katika vipaumbele vyake ni demokrasia, kutenda haki na kuisimamia serikali kutekeleza ilani za uchaguzi.

Kuhusu demokrasia, alisema jambo kubwa ni kuimarisha demokrasia ndani ya chama ikiwamo haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

"Lazima haki ya kuchaguliwa na kuchagua ipatikane bila rushwa, mizengwe wala umaarufu, rushwa na upendeleo. Pia haki ya kutoa mawazo, ni lazima wanachama wawe na haki ya kutoa mawazo. Hakuna mwenye hakimiliki ya kutoa mawazo.

"Hata uamuzi ukifikiwa na hukuupenda lazima uuheshimu Wanachama wakimchagua mtu, CCM ni nani wa kumpinga? Inawezekana kukatokea sababu za kimaadili lakini kimsingi tusimamie dekomrasia, tulinde haki," alisema.

Kinana pia alisema haki ikiimarishwa ndani ya CCM ni rahisi kuimarishwa pia nje ya CCM.

"Rais anazungumzia suala la haki. Hata wakati anapokea ripoti ya CAG alisema vyeti pekee si sifa, maana yake vyeti viende na uadilifu na sifa na uzoefu, uhodari na wakati mwingine viende na kukubalika," alisema.

Alisema Tanzania inajulikana hata nje ya nchi kwa kutenda haki, hivyo wanachama na viongozi wa CCM wanapaswa kuwa mfano wa kusimamia na kuteteta haki pamoja na kukataa dhuluma.

Katika hatua nyingine, Kinana alionya kuwa serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar ni za CCM, hivyo hazipaswi kuiagiza CCM bali kupokea na kutekeleza maagizo kutoka kwenye chama,

"CCM si mali ya serikali bali serikali hizi zinatokana na CCM. CCM hatupokei maelekezo toka serikalini. Serikali haiagizi CCM bali CCM inaziagiza serikali kupitia sera zake, ilani zake na ahadi zilizotolewa na viongozi mbalimbali wakati wa uchaguzi. Wanaokwenda kuomba kura si serikali ni CCM. Msithubutu kutunyang'anya hiyo haki.

Kazi ya kusimamia sera, ilani, maelekezo ni ya Chama Cha Mapinduzi. Pale serikali inapofanya vizuri, kila mwana CCM ana wajibu wa kuisifia. Kunakpokuwa na kasoro wana CCM tuna wajibu wa kuwasemea wanachi kuhusu kasoro hizo.

"Tusiseme kwa kukejeli serikali, tuna vikao vya chama. Viongozi wa serikali wako kwenye vikao vyetu vya chama tunazungumza nao, tunawaambia, tunawaelekeza yale yaliyomo kwenye ilani," alisema.

Pia alisema si sawa kwa mwana CCM kwenda hadharani kuisema serikali kwa kuwa kila miezi sita hukutana na kujadili ilani na hapo ndipo panapofasa kueleza kasoro na mazuri yaliyomo.

"Chama hiki ni kikubwa na kina historia. Penda usipende chama hiki kinakubalika na Watanzania, hivyo lazima CCM ibaki kuwa masikio ya wananchi. Tuwatembelee wananchi kwenye maeneo yao, tuwasikilize, tujenge utamaduni wa kuwasikiliza na kuwatembemea," alisisitiza.

Alisema kwa kufanya hivyo wataichagua kwa sababu wanajua chama kinajali shida zao na kinazifanyia kazi kwa kuzitatua.

Kinana pia aliahidi kutembelea mikoa na wilaya kuzungumza na wananchi kwa niaba ya mwenyekiti kama katiba inavyoelekeza.

"Nashukuru kwa imani yako, umenipa nafasi kujiunga na ligi ya watu watu wazito. Kawawa, Msekwa, Mangula na sasa mimi. Ninajiunga na hiyo mila nilikuwa Katibu sasa Mwenyekiti. Namtakia kila la heri Chongolo awe Mwenyekiti Makamu," alisema.

## Wakongwe walivyomnadi Kinana

**Na Epson Luhwago,** DODOMA

WANASIASA wakongwe, Stephen Wasira, Mberwa Hamad Mberwa na Yussuph Makamba, jana walimwagia sifa Makamu Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, wakati wakimnadi ili achaguliwe katika nafasi hiyo.

Hatua ya wanasiasa hao ilisababisha wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalumu wa Taifa wa CCM kulipuka kwa shangwe na vigelegele kila walipokuwa wakizungumza.

Waziri wa zamani katika serikali za awamu ya kwanza, ya pili na ya nne, Stephen Wasira, alikuwa wa kwanza kumwaga sifa hizo, akisema Kinana anafaa kutokana na nafasi aliyopendekezwa kugombea kuwa nyeti.

"Nafasi anayogombea au ameteuliwa ili apigiwe kura ni nyeti sana. Rais (Samia Suluhu Hassan) ambaye ni mwenyekiti ana kazi nyingi sana. Akiachiwa atahemewa ndiyo maana wakawekwa makamu wenyeviti wawili wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

"Kwa hiyo, Kinana anachaguliwa kuchukua nafasi ya kumsaidia mwenyekiti, ndiyo maana imeandikwa kuwa atafanya kazi zote atakazotumwa na mwenyekiti," alisema Wasira.

"Sasa Kinana ni nani Mpaka tunampa jukumu kubwa hili? Alizaliwa Arusha miaka 71 iliyopita. Ana elimu ya kawaida aliyoipata Chuo Kikuu cha Yugosilavia na Chuo Kikuu cha Harvard, Marekani katika sayansi ya siasa na uhusiano wa kimataifa. Pia amefanya kazi Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa miaka 20 hadi alipostaafu mwaka 1992 akiwa na cheo cha kanali," alibainisha.

Wasira pia alisema Kinana aliwahi kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kabla ya hapo alikuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Alisema Kinana aliwahi kuwa Mbunge wa Arusha Mjini kwa miaka 10 hadi mwaka 1995 alipoamua kung'atuka. Pia alisema alikuwa Spika wa kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki mwaka 2001 hadi 2006.

"Ndani ya chama pamoja na kushika nafasi ya Katibu Mkuu, amekuwa mjumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa miaka mingi mpaka nashindwa kuhesabu," alisema.

Akiwa Katibu Mkuu, Wasira alisema mwaka 2012 wakati chama kinapita katika misukosuko, Kinana na sekretarieti yake walisafiri mikoa yote ya Tanzania kukinusuru chama na kukirekebisha katika mstari wake.

"Katika kipindi hicho, kuliibuka msamiati wa mawaziri mizigo na Kinana alifanya kazi ambayo ilisababisha Rais (Jakaya Kikwete wakati huo) kufanya mabadiliko makubwa yaliyowaondoa wale walioitwa mizigo," alibainisha.

"Baada ya kuwa namjua na ninyi mnamjua, tatizo sasa liko wapi? Nawaomba wajumbe kumchagua kwa nafasi hii. Wangapi wamenielewa?" alimalizia Wasira huku wajumbe wakijibu "woteeee."

ANA BUSARA, MCHAPAKAZI

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mbwerwa, alimwelezea kinana kuwa ni mtu mwenye busara, mchapakazi na mtu mkarimu.

"Kinana ni mtu ambaye ana busara ya hali ya juu katika kukabili mambo, Pia ni mchapakazi asiyejali muda, bali kazi yake iende vizuri.

Lakini kubwa zaidi, ni mtu mkarimu sana na siku zote mtu mkarimu Mwenyezi Mungu anakuwa karibu, Nawaomba wajumbe wenzangu tumkubali Kinana kwa nafasi hii. Mwenyekiti (Rais Samia Suluhu Hassan) akipata mtu mkarimu kama yeye, chama kitasonga mbele," alisema.

Mberwa pia alisema alimfahamu kwa undani Kinana wakati wa mgogoro wa kisiasa baina ya John Mwakipesile na Dk. Harrison Mwakyembe mkoani Mbeya kwa kutatua mgogoro huo uliokuwa umewagawa wanachama katika makundi.

"Tulikuwa mimi, Kinana na Pindi Chana tulioteuliwa kwenda kutatua mgogoro ule. Ulikuwa mzito lakini Kinana kwa busara zake aliwezesha kumalizika ndani ya saa nne tu. Mpaka leo kule Kyela ni shwari," alisema.

**NI MNYENYEKEVU**

Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Makamba, alisema pamoja na kufanya kazi wakiwa ofisi moja Korogwe, Kinana ni mtu wa kujishusha na hapendi makuu.

"Baadaye tulikutana Monduli (chuo cha kijeshi) akiwa mwalimu wetu mimi na Jakaya Kikwete. Siku moja tulichokozwa na mwenzetu mmoja tukataka kuchukua hatua lakini alipokuja alitutuliza kwa kutuambia walituchokoza ili wajue 'emotion' zetu.

"Lakini wakati wa vita vya Kagera akiwa kanali, mimi luteni, alinitaka mimi nikae mbele jambo ambalo ni vigumu. Huyu ni mtu rahimu, anajua kujishusha," alisema.

Pamoja na kuwataka wajumbe kumpa kura zote za ndiyo, alimtaka Kinana kuwasamehe wale wote waliomtupia madongo na kufanya mambo kwa ajili ya kukijenga chama.

"Msamaha ni silaha ya watu imara. Mimi na Kinana tulifikishwa kwenye Kamati ya Maadili na tukasamehewa. Watu walitutupia madongo. Sasa wewe leo ndiye bosi wao, uwasamehe," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mrema, mkewe waamsha shangwe mkutano CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Augustino Mrema, na mke wake, Doreen, jana waliamsha shangwe kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika mkutano huo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini hapa, Mrema na mkewe ambao walifunga ndoa hivi karibuni, waliingia wakati mkutano unaendelea.

Shangwe hizo zililipuka wakati Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa hotuba yake ya ufunguzi.

Akiwa katika ufunguzi huo, Rais Samia alishtushwa na shangwe za wajumbe wa Mkutano Mkuu ndipo akasema: "Bwana harusi na bibi harusi hoyee" na wajumbe wakaitikia "hoyeeee..."

Baada ya kumaliza hotuba yake ya ufunguzi, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Shaka Hamdu Shaka, alitoa utambulisho kwa kusema: Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na kwamba utambulisho ulishafanyika, ninaomba niwatambulishe wageni waliofika hivi punde ambao ni Mrema na Mama Mrema."

Mrema alikuwa miongoni mwa viongozi wa vyama vya siasa waliohudhuria mkutano huo sambamba na wa vyama vya Sauti ya Umma (SAU), NSSR-Mageuzi, NDL, UPDP, ADA Tadea, UDP, Demokrasia Makini na ADC.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na viongozi wastaafu wa CCM, mabalozi wa nchi mbalimbali, viongozi wa dini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na wahariri wa vyombo vya habari.

# Makamba ampigia debe Samia 2025

**Na Epson Luhwago,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Yussuph Makamba, amempigia debe Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ndiye anayefaa kwa urais mwaka 2025.

Makamba alisema hayo jana alipopewa nafasi ya kumzungumzia aliyekuwa mgombea wa nafasi ya makamu mwenyekiti wa chama hicho, Abdulrahman Kinana.

"Jakaya (Kikwete) aliwahi kumwambia Mzee (Pius) Msekwa kuwa mimi ni toboa tobo. Sasa leo (jana) natoboa tobo.

"Hivi karibuni nilikusikia ukizungumza na wanawake wote Tanzania ukisema hawajamchagua Rais mwanamke bali watamchagua mwaka 2025.

Sasa natoboa mwanamke huyo ni wewe.

Sasa kama kuna mpinzani anajiandaa, mwambieni ajiweke pembeni," alisema.

Makamba alisema Rais Samia ni kocha mzuri na kwa timu yake mwaka 2025 kuna ligi na magoli ya ushindi yataingia kwa sababu tuna kocha mzuri na Kinana anachaguliwa kuwa kocha msaidizi ndani ya chama kwa ajili ya ushindi 2025," alisema.

Pia alisema alipopata taarifa za Samia kuwa Rais, alisema alimtabiria kuwa ujio wake ni 'ubatizo wa maji na faraja' kwa kuwa wananchi wanapata huduma mbalimbali.

"Ni kweli mama (Samia) unatufariji kwa sababu maji tunapata, watoto wetu wanasoma na mikopo tunapata," alisema.

Awali, Makamba alisema Samia alipoteuliwa kushika madaraka ya urais, alimtumia ujumbe wa maandishi kumpongeza huku akisema ndiye amechaguliwa na Mungu kushika wadhifa huo.

"Mungu amefanya uongoze Tanzania kwa majira haya.

Na nilisema asante Mungu kwa hilo. Wako wengi wanaofaa lakini wewe ndiye unafaa zaidi.

Aliongeza kuwa: "Lakini niliomba uwe na mabega makubwa uubebe mzigo huu (urais). Kuna msemo kwamba mzigo mkubwa mpe Mnyamwezi lakini hata Mkwere (Jakaya Kikwete) aliubeba, sasa Mzanzibari atashindwaje?" Makamba alihoji na kuibua vicheko ukumbini.




Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiserebuka kwa furaha, wakati wa mkutano huo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu za Philip Mangula kung'atuka uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula, amesema ameng'atuka uongozi lakini ataendelea kuwa mwanachama mtiifu na mzalendo kwa nchi yake.

Mangula alisema hayo muda mfupi baada ya kupatikana kwa mritihi wake kutokana na uchaguzi uliofanyika jana.

Alisema ataendelea kutoa mawazo yake na mchango kwa ajili ya maendeleo ya chama huku akibainisha kuwa licha ya kung'atuka, anaendelea kuwa mjumbe katika kamati ya ushauri inayoundwa na viongozi wastaafu.

Mangula alisema kazi ya mafaili amemwachia Kinana huku akidai kuwa walishaanza kuwaweka kwenye faili wale wanaochungulia 2025.

"Komrade Kinana alizoea kuniita SG, yeye mwenyewe sasa ni SG, katika mabadiliko ya Katiba tuliyobadilisha bahati nzuri kanuni ya uongozi na maadili ni zile zile, hazijabadilika na komrade Kinana anazijua.

"Ile kamati ndogo ile ya maadili ile ya kuhoji sasa nimeacha mafaili hayo nakukabidhi ndugu Kinana, sasa ndiyo mzee wa mafaili. Mzee wa mafaili huwa tunaweka kumbukumbu? wanaochungulia 2025 nilishaanza ukiona tu kuna dalili fulani fulani unafungua faili unaanza kuweka kumbukumbu.

"Huyu kasemwa huku weka hapa, ana mtandao huu weka hapa, kila mmoja anayeonekana kukiuka taratibu namfungulia faili ili uweke kumbukumbu zake zote za mambo anayoenda kinyume cha maadili aliyofanya.

"Ukifika wakati unamwita njoo ulikiuka kanuni hizi tarehe hii na kadhalika, ndiyo sababu ya kuitwa mzee wa mafaili, sasa nimemkabidhi Kinana," alisema.

Katika barua aliyoiwasilisha juzi, Mangula alisema sababu za kuchukua uamuzi huo huku akibainisha kuwa ni umri na utumishi wake wa muda mrefu ndani ya chama na serikali.

"Nimeamua kung'atuka na uamuzi huu unatokana na sababu za umri, utumishi wa muda mrefu, hivyo kushindwa kutimiza majukumu yangu. Ifikapo leo (juzi) Machi 31, nitakuwa natimiza miaka 81," alisema katika barua hiyo.

Mwenyekiti wa CCM Taifa, Samia Suluhu Hassan, alisema katika barua hiyo, Mangula alisema alianza utumishi Januari Mosi, 1962 wakati huo yeye Akiwa na miaka miwili.

Mangula alianza kazi akiwa mwalimu na baadaye kuwa mwalimu wa Chuo cha Chama Kivukoni (sasa ni Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere), akiwa mmoja wa makada 75 walioteuliwa na chama tawala- TANU enzi hizo.

Akiwa mwalimu wa chuo hicho, pia alikuwa mhariri wa magazeti ya chuo hicho, Ujamaa na Mbioni na kuendesha mafunzo ya masafa kupitia iliyokuwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD- sasa TBC) katika vipindi vya Fimbo ya Mnyonge na Ukombozi Kusini mwa Afrika.

Pia aliwahi kuwa mshauri wa wanafunzi chuoni hapo kabla ya kuteuliwa kuwa naibu mkuu wa chuo kwa miaka sita.

Baada ya utumishi huo, aliteuliwa kuwa katibu wa tanu wa wilaya sambamba na mkuu wa wilaya wakati huo kukiwa na kofia mbili. Baadaye aliteuliwa kuwa mkuu wa mkoa katika mikoa mbalimbali kwa miaka 11.

Mwaka 1997 aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM, nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2006 na nafasi yake kuchukuliwa na Yusuph Makamba.

Katika barua yake hiyo, Mangula alisema ni wakati mwafaka sasa wa kukisuka na kukiimarisha chama kwa kupanga safu mpya za uongozi. Alishauri chama kumteua mwanachama mwingine kujaza nafasi yake ambaye ataongeza nguvu katika malengo na madhumini yake.

Kutokana na barua hiyo, Rais Samia alisena Kamati Kuu (CC) ilikaa na kujadili hatimaye kumpendekeza Kinana na baadaye NEC kuridhia na kuagiza jina hilo lipelekwe kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM kwa ajili ya kupigiwa kura.

Baada ya kutangaza jina hilo na kutoa rai kwa wajumbe, Tanzania One Theatre (TOT) walidakia kwa wimbo wa "Sasa kumekucha, jogoo limekwishawika Dodoma, kada wa CCM apewe kura za ndiyo... yuko wapi, yule pale ndugu Kinana..."

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

JOACHIM REVOCATUS WIBOGA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA LANDCRUISER yenye namba za usajili T971 BDU, CHASSIS NAMBA: HDJ810050981, ENGINE NAMBA: IHD0095892. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/131094/2022

# Wizara hii kaa la moto, miaka 60 mawaziri 24

**Na Romana Mallya**

JUZI Rais Samia Suluhu Hassan alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri huku mawaziri watatu wakibadilishwa.

Walioguswa na mabadiliko hayo ni George Simbachawene, Waziri wa Katiba na Sheria aliyehamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu), Dk. Damas Ndumbaro, Waziri wa Maliasili na Utalii aliyehamishiwa Wizara ya Katiba na Sheria na Balozi Pindi Chana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu) aliyepelekwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kuondolewa kwa Dk. Ndumbalo Wizara ya Maliasili na Utaliii ni mwendelezo wa historia ya mawaziri kutokaa kwa muda mrefu katika wizara hiyo na Dk. Chana ameweka rekodi ya kuwa waziri wa 24 kuitumikia wizara hiyo tangu uhuru wa nchi.

Orodha ya mawaziri katika wizara hiyo ilianza mwaka 1962, yaani miaka 60 iliyopita Waziri wa kwanza akiwa ni Tewa Said aliyeongoza hadi mwaka 1965, alipomwachia kijiti Derek Bryceson aliyekaa wizarani hapo hadi mwaka 1970 alipokabidhi ofisi kwa Hassan Makame, naye akaitumikia kwa miaka mitano hadi mwaka 1975.

Waliofuata ni: Solomon Ole Saibul (1975-1980); Isaack Sepetu (1980-1982); Ali Hassan Mwinyi (1982-1983); Sir George Kahama (1983-1984); Paul Boman (1984-1985); Getrude Mongella (1985-1987).

Arcado Ntagazwa (1987-1989), akilaumiwa kwa kitendo cha ubinafsishaji wa hoteli kwa bei ya chini zilizokuwa zinamilikiwa na serikali; Marcel Komanya (1989-90); Abubakar Mgumia (1990-1993) akikumbana na kero ya uharibifu wa misitu kutokana na biashara ya mbao iliyokuwa ikifanyika wakati huo.

Juma Hamad Omar (1993- 1995) alikabiliwa na kashfa ya wizara kuuza Pori la Loliondo kwa mwana wa Mfalme wa Falme za Kiarabu iliyosababisha kuundwa kwa Kamati ya Bunge iliyoongozwa na Mateo Qaresi na aliondoka wizarani baada ya Rais Benjamin Mkapa kuingia madarakani.

Juma Ngasongwa (1995-1996) alijiuzulu baada ya kashfa ya biashara ya minofu ya samaki kuuzwa nje ya nchi bila kulipa kodi; Zakhia Meghji (1997-2005) akikaa wizarani hapo kwa muda mrefu na moja ya sifa kubwa aliyojipatia ni kitendo chake cha kuutangaza utalii kwa kiasi kikubwa.

Anthony Diallo (2005-2006); Prof. Jumanne Maghembe (2007-2008);

Shamsa Mwangunga (2008-2010); Ezekiel Maige (2010-2012) aliondolewa katika nafasi hiyo baada ya maagizo ya Bunge kutokana na kuibuka kwa kashfa ya uuzaji wa wanyama hai.

Khamisi Kagasheki (2012-2013) wakati wake alijipatia sifa kubwa kutokana na jitihada zake za kupambana na vitendo vya ujangili; Lazaro Nyalandu (2014-2015) ni waziri aliyeongoza wizara hiyo hadi Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na Rais Magufuli alipotangaza baraza lake la kwanza la mawaziri Desemba 2015 alimrudisha Prof. Maghembe ambaye Oktoba 2017 aliacha kwa Dk. Khamis Kigwangalla aliyeongoza hadi Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 lakini hakurejea kwenye Baraza la Mawaziri baada ya uchaguzi huo, kiti chake kilichukuliwa na mtaalamu wa sheria, Dk. Ndumbaro.

## Samia aonya rafu uchaguzi wa CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, amekemea ukiukwaji maadili ya uchaguzi wa ndani ya chama.

Alitoa onyo hilo jana kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM wa Taifa ambao ulikuwa na ajenda mbili za Mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 Toleo la 2020 na uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara.

Alisema mwaka jana CCM iliitisha mkutano kama huo ambao ulimchagua kuwa Mwenyekiti na aliahidi mambo mbalimbali ikiwamo kuongoza chama kwa kuzingatia katiba, kanuni na taratibu.

Rais Samia alisema mwaka huu kuna uchaguzi ndani ya chama hicho na kutaka uendane na hali halisi ya mifumo ya siasa nchini na kuwahamasisha vijana na wanawake kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi huo ngazi zote.

Alizitaka kamati hizo kusimama kwenye njia za haki huku akisema katika uchaguzi huo marekebisho ya Katiba yaliyofanyika yatazingatiwa.

"Ahadi yangu kwenu ni kukitumikia chama na kujijenga katika ubora na madhubuti yake, nasema nikitambua kuna mabadiliko ya siasa ndani ya dunia na nchi yetu kwa hiyo lazima CCM ibadilike kuendana na siasa zinavyobadilika, tunafanya mabadiliko kuendana na mifumo ya siasa inavyokwenda,"alisema.

**WAJUMBE WAREJESHWA**

Kuhusu marekebisho ya katiba, Mwenyekiti Samia alisema madhumuni ya marekebisho hayo ni kuongeza kasi na ufanisi wa kazi za chama na utekelezaji wa uamuzi wa vikao vya chama.

"Tumerudisha makatibu wa mikoa ndani ya NEC ili kuongeza kasi ya utekelezaji ili wapate maelekezo ndani ya NEC na sio kusubiri wanaotoka wakawaambie, na wasipowajibika tuwaseme na kuwawajibisha pale.

"Pia kuongeza usimamizi na uthibiti wa chama kwa viongozi wake wanaochaguliwa katika utekelezaji wa ilani na mamlaka za serikali za mitaa ndio maana uteuzi wa mameya utafanywa na Kamati Kuu ili tuweze kuwadhibiti vizuri,"alisema.

Vilevile, marekebisho yamelanga kuimarisha nguvu za chama katika kukabiliana na vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

"Tumelenga kuongeza uwakilishi wa jumuiya za CCM, ngazi ya kata kwenye Mkutano Mkuu wa CCM Wilaya na kurekebisha itifaki ya uwakilishi unaofanana na wenyeviti na makatibu wa jumuiya za CCM ngazi ya mkoa kuwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa na Mkutano Mkuu wa Mkoa," alisema.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Daniel Chongolo, ibara 12 zimeguswa na marekebisho hayo ya katiba.

# Mbaroni tuhuma za kujitengenezea tukio la kuvamiwa na majambazi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia mfanyabiashara Ally Musa (36), kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo polisi kuwa amenyang'anywa Shilingi milioni nane na watu waliokuwa na silaha wakati fedha hizo alitapeliwa wakati akitaka kuzibadilisha kuwa Dola.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema mfanyabiashara huyo aliliambia Jeshi la Polisi kuwa fedha hizo aliporwa wakati akizipeleka benki.

"Mfanyabiashara huyu alitoa taarifa za uongo kuwa alinyang'anywa Sh. 8,000,000 maeneo ya Temeke Mwembe Yanga, wakati akizipeleka benki ya CRDB Temeke Stereo, ambako alidai ghafla alivamiwa na watu sita wakiwa kwenye pikipiki tatu, mmoja akiwa na silaha ndogo," alisema.

Kamanda Muliro alisema, Mussa alidai watu hao walimshambulia na kumpora fedha hizo zilizokuwa ndani ya begi.

"Jeshi la Polisi lilifanya uchunguzi wa kina wa tukio hili na ilibainika kuwa hakukuwa na unyang'anyi wa kutumia silaha bali lilikuwa tukio la kutengenezwa na mtoa taarifa, ilibainika fedha zile alipewa na tajiri yake ili azipeleke benki na njiani aliingiwa na tamaa akatapeliwa baada ya kutaka kupata Dola za Marekani kwa kubadilishana na hizo alizokuwa nazo," Muliro alisimulia.

Alisema mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani kwa kutoa taarifa za uongo kwa ofisa wa serikali.

Katika tukio lingine, Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limemkamata Mohamed Omary (27), mkazi wa Chamazi kwa tuhuma za kushiriki katika matukio ya unyang'anyi wa pikipiki kwa waendesha bodaboda kwa kushirikiana na wenzake wawili, Athuman Abdallah, mkazi wa Yombo na Hassan Twaha, maarufu Dangote mkazi wa Mtongani Temeke.

"Watu hawa wamekuwa wakitumia mbinu ya kuiba pikipiki kwa kumtumia mwanamke ambaye hujifanya mjamzito, Aziza Hamza (21) mkazi wa Yombo ambaye hukodi bodaboda mpaka walipo wenzake kwa ajili ya kutekeleza wizi," alisema.

Kamanda Muliro alisema baada ya kufanikisha huzipeleka pikipiki hizo kwa Omary Salum (30), mkazi wa Tandika, Kilimahewa ambaye kazi yake ni kutoa GPRS/ ving'amuzi kwa pikipiki zenye ving'amuzi.

"Athuman Mohammed Bakari, maarufu Boko, mkazi wa Kilwa Kivinje, huzitafutia kadi na kuziuza katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Tumemkamata Sophia Musa (28), mkazi wa Toangoma, ambaye ndiye mpokea maombi ya kutengeneza kadi kutoka kwa Boko na baadaye kumpelekea Ibrahimu Ally, mkazi wa Buguruni ambaye hufanya kazi ya kudurufu kadi hizo," alisema.

Kamanda Muliro alisema, katika upekuzi uliofanyika watuhumiwa hao wamekutwa na pikipiki tatu za wizi, kadi za pikipiki tisa, kadi za gari 11, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumaliza elimu ya sekondari, stika za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na stika za Baraza la Mitihani.

Katika tukio lingine, Kamanda alisema polisi kwa kushirikiana na TRA wanachunguza wamiliki wa pikipiki nane ambazo madereva wake walikimbia na kuzitelekeza zinazotumika kupora mikoba katika maeneo mbalimbali ya jiji.

"Pikipiki hizo zina namba za usajili MC.928 CWC, MC. 685 CRR na MC. 304 DCR, zote aina ya boxer na nyingine Fekon ambayo namba zake zimekatwa.

Alisema nyingine nne ambazo hazijasajiliwa zenye chesisi namba pekee ni MD2B15BY3LWK85620, MD2A21BY4KWA96154, MD2A21BY5JWH87188, zote aina ya boxer na nane ambazo chesisi zake zimefutwa.

Katika tukio lingine, jeshi hilo linawashikilia watu wanane wanaotuhumiwa kwa vitendo vya uvunjaji na kuiba vitu mbalimbali katika maeneo ya Kimara, Mabwepande, Mbweni na Kinondoni.

Pia, Kamanda Muliro, alisema wanawashikilia watu wawili kwa tuhuma za wizi wa magari.

Alisema Jeshi la Polisi limewakamata watu wengine wawili wanaotuhumiwa kuiba gari aina ya Suzuki Cary yenye chesisi namba DA52T128686 lililoibwa Machi 27, mwaka huu.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

JOSEPHAT FRANCIS MALLYA anatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 945 CUY aina ya TOYOTA PROGRESS, yenye Chassis no. JCG100013429 na Engine no.1JZ234165. Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. TAARIFA YA POLISI: KAH/TR/RB/189 /2022.

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**

DOREEN EMMILY MREMA anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba TAE 096935 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. CONTROL NUMBER: 9910832475866

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

CIMPAYE JACQUES CIMPAYE anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari(isuzu) yenye namba za usajili T 855 DQR, CHASSIS NO.UBS73GW7202414,ENGINE NO.4JX1510589 yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0778463156 POLISI TAARIFA: MOR/MOR/RB/132315/2022

# Machinga wakumbukwa bima maalumu majanga

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Howden Puri imezindua bima maalumu kwa wajasiriamali ijulikanayo kwa jina la Hifadhi Biashara, inayolenga kulinda wafanyabiashara wadogo wanapopata majanga mbalimbali.

Kupitia Hifadhi Biashara, mfanyabiashara anaweza kuweka kuanzia Sh. 7,000 kwa mwezi ili kulinda mtaji wake endapo atapata majanga kama ya moto, wizi na kupata fidia hadi Sh. milioni tano ili kuendelea na biashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Howden Puri, Umesh Puri, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, alisema wameamua kuweka bima ya gharama nafuu ili kuwawezesha wafanyabiashara wengi kujiunga na kuwa na matumaini ya kuendelea na biashara zao.

Alisema kwa kawaida gharama za bima ni ghali na kusababisha wafanyabiashara wadogo kushindwa kujilinda na majanga mbalimbali.

Alifafanua kuwa kampuni yao imeona tatizo hilo na kuja na utatuzi kwa wafanyabiashara hao kupitia maendeleo makubwa ya teknolojia kujiunga na bima kuwa rahisi na kupatikana muda wote.

"Mfanyabiashara hahitaji kwenda ofisini kujiunga na huduma ya Hifadhi Biashara zaidi ya kutumia simu ya kiganjani kupitia TigoPesa USSD code *150*01#, app ya duka.direct na Selcom kupitia wakala yeyote nchini," alisema.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyabiashara Wadogo (Machinga) Mkoa wa Dar es Salaam, Yusuph Namoto, alisema wafanyabiashara wengi walitetereka na wengine kufilisika wakati wa janga la UVIKO-19 na moto katika masoko ya Kariakoo, Karume na Mwenge.

Namoto alisema bima ya Hifadhi Biashara ni suluhisho la majanga yote kwa wafanyabiashara na kuwaomba kujiunga na kuwaomba kampuni ya bima kutoa huduma bora za madai wanapoletewa.

Mkuu wa Kitengo cha Tigo-Pesa, Mshamma Mshamma, alisema wameamua kuingia katika huduma hiyo kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kufanya huduma ya kulipa na kupokea malipo kupitia mtandao bora zaidi.




Mkuu wa wilaya ya Ilala, Ng'wilaburu Ludigija (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa Bima ya Hifadhi Biashara, iliyoanzishwa na kampuni ya Howden Puri, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahitimu vyuo vikuu wawekewa mikakati kujiajiri

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

VIJANA wanaohitimu vyuo vikuu na vya kati nchini sasa watakuwa na uhakika wa kujiajiri katika sekta za kilimo, uvuvi na mtambuka, baada ya taasisi isiyo ya kiserikali ya kuhamasisha ujenzi wa uchumi, viwanda na utafutaji wa Rasilimali Fedha za Miradi (DEVCOM), kuanza mpango wa kuwasaidia kuanzisha kampuni.

Kupitia mpango huo, DEVCOM imelenga kuweka mikakati, hadi kufikia mwaka 2026 kuwe kumeanzishwa kampuni zaidi ya 100 ya vijana wahitimu wa vyuo vikuu, vya kati na vya ufundi ambavyo vitasaidia kuongeza ajira.

Akizungumza katika kongamano linalohusisha vyuo vya elimu ya juu, kati na Ufundi na wadau mbalimbali, Mtendaji Mkuu wa DEVCOM, Gaston Kaziri, alisema mradi huo umekuja kutokana na wahitimu wengi kukosa ajira baada ya kuhitimu.

Alisema vyuo vimekuwa vikifanya juhudi za kutoa stadi za ujasiriamali, lakini kuna haja ya kufanya jitihada zaidi ya kuwa na miradi ya mikakati ili kusaidia vijana walio vyuoni na waliomaliza vyuo kujiajiri wenyewe.

Alisema kupitia mradi huo kwa pamoja wataangalia namna ya kuwasaidia vijana wanaomaliza vyuo hivyo kwenda kwenye ajira ya kujitegemea.

"Kongamano hili linakwenda kusaidia wanafunzi wa vyuo vikuu na wahitimu ili waweze kujiajiri kwa kuanzisha kampuni katika sekta ya mtambuka ikiwamo kilimo," alisema Kaziri.

Alisema mpango huo umekuja kutokana na wahitimu wengi kupata changamoto wanapotaka kuanzisha kampuni yao wanashindwa kukopesheka na taasisi za fedha kutokana na kukosa dhamana.

"DEVCOM haitoi fedha bali inawasaidia kutambua wapi kuna fedha na kuhakikisha hizo fedha wanazipata kwa njia ya mkopo ama kwa njia nyingine zinazotokana wafadhili wa maendeleo," alisema Kaziri."

Alisema kutokana na changamoto wanazozipata, Shirika la DEVCOM limeamua kuwaweka pamoja ili wawe na vikundi vitakavyowasaidia kuanzisha kampuni yao na shirika hilo liwasaidie kwenye mchakato wa uanzishwaji wake.

Alisema serikali imeweka malengo ya kutengeneza ajira milioni saba hadi kufikia 2020/25, na jukumu hilo haliwezi kuiachia serikali pekee lazima kama sekta binafsi wana jukumu la kuisaidia serikali ili kufikia lengo hilo.

"Wafadhili au Taasisi haiwezi kukupa fedha kwa kuwa wewe umemaliza chuo kikuu bali ni lazima uonyeshe ni nini ulishakianza ikiwamo miradi midogo," alisema.

Mshauri wa masuala ya uwekezaji wa shirika hilo, Dk. Kilontsi Mporogomyi, alisema imefika wakati sera ya serikali katika masuala ya kilimo ikiwa ni sekta muhimu katika taifa kubadilika kwa kukihudumia kilimo ili kuleta maendeleo zaidi.

"Tukienda kwenye Tanzania ya viwanda inawezekana ikiwa kilimo tutakikumbatia, tutakiwezesha na kama kitafanya vizuri zaidi ili kuwezesha maendeleo ya viwanda," alisema Dk. Mporogomyi.

Akizungumzia nafasi ya vijana wengi ambao hawana ajira baada ya kuhitimu vyuo vikuu, alishauri serikali kuanzisha taasisi za kifedha zitakazowezesha kupata mikopo yenye riba ndogo tofauti na benki.

Baadhi ya wahitimu wa vyuo vikuu walioshiriki katika kongamano hilo, Jedica Leonidas kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, alishauri wasomi vijana wabadili mitazamo kwa kutambua elimu waliopata waitumie pia kwa kufanya shughuli za ujasirimali ili kukuza uchumi.

# Mamlaka ya Elimu Tanzania TEA yafadhili miradi 3,314 ya elimu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imefadhili miradi 3,314 ya elimu yenye thamani ya Sh. bilioni 212.6 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Bahati Geuzye, alitoa takwimu hizo wakati akifungua semina ya siku moja kwa waandishi wa habari kuhusu majukumu ya TEA.

Alisema kwenye fedha hizo, Sh. bilioni 200 zilitolewa kama ruzuku na Sh. bilioni 12 zilitolewa kama mikopo nafuu kwa shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu.

Alisema miradi hiyo imejumuisha ujenzi wa mabweni 73, vyumba vya madarasa 1,050, matundu ya vyoo 5,880 na nyumba za walimu 560 katika shule 791 za msingi na sekondari.

Mkurugenzi alisema, TEA imeratibu ukarabati wa shule 17 za sekondari kongwe, ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa kwa shule 71 za msingi na sekondari zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Alisema TEA pia ilifadhili mafunzo maalumu ya kuongeza uwezo wa kitaaluma wa wanafunzi 2,196 wa kike, kuiwezesha Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), kuandaa na kuchapisha mihutasari, mitaala na vitabu vya kiada kuanzia darasa la tatu mpaka la sita kwa shule za msingi. Alisema miradi mingine iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa kwa vyuo vikuu ambavyo ni Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere (MJNUAT), Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume (KIST), Taasisi ya Utawala wa Umma (IPA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema katika mwaka wa fedha 2014/15 na 2015/2016, TEA ilitoa ufadhili wa mafunzo ya kujenga uwezo katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa ambao ulifadhili mafunzo ya kujenga uwezo kwa walimu wakufunzi 1,572, walimu wa shule za msingi 36,876 wa masomo ya Kiswahili, Hisabati na Kiingereza.

Alisema walitoa mafunzo kwa walimu 6,000 wa shule za sekondari wa masomo ya Biolojia, Kiswahili, Hisabati na Kiingereza pamoja na Kuwezesha Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), kupanga matokeo ya ufaulu, na kuchapa vitabu vya maswali ya mitihani.

"Katika kuunga mkono jitihada za serikali za kuhamia Dodoma na ongezeko la watumishi wa umma na wananchi kuhamia katika mji mkuu wa Dodoma, TEA iliona kuna umuhimu wa kuboresha na kukarabati baadhi ya shule za msingi ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi katika mji huo Mkuu," alisema. Alisema, mradi huo ulilenga kukarabati na kupanua miundombinu ya shule za msingi Kizota, Medeli, Kisasa na Mlimwa C.

Alisema kupitia Mfuko wa Elimu, katika mwaka wa fedha 2021/2022 zaidi ya Sh. bilioni 8.6 ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharimia ufadhili wa miradi 160 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule 151 nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mungu ibariki Simba SC katika michuano ya CAF*

**MASHABIKI** wa soka nchini kesho wataelekeza macho na masikio yao kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuwafuatilia wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba watakaposhuka dimbani ugenini kuwakaribisha US Gendarmarie kutoka Niger.

Mechi hiyo ni ya mwisho katika hatua ya makundi, Simba ilipangwa katika Kundi D pamoja na timu za RS Berkane ya Morocco na Asec Mimosas kutoka Ivory Coast.

Bila kusubiri matokeo mengine, Simba iliyoanza hatua ya makundi kwa ushindi mnono wa mabao 3-1 dhidi ya Asec Mimosas, kesho inahitaji ushindi na kuendeleza rekodi yake safi ya kuvuna pointi zote inapocheza kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Benjamin.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatakiwa kuingia katika mchezo huo kwa nidhamu na tahadhari ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Tunawakumbusha wachezaji wa Simba kuendelea kupambana kwa kucheza katika kiwango bora kama walivyofanya kwenye mechi michezo mingine iliyopita na hatimaye watapata kile ambacho wanakihitaji.

Inafahamika wazi kusonga mbele kwa Simba katika michuano hiyo, si tu kutainufaisha klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini, lakini itaendelea kuipa Tanzania nafasi ya kutoa timu nne kwenye mashindano ya CAF katika msimu ujao.

Simba haitakiwi kuingia uwanjani ikiwadharau US Gendarmerie, eti kwa sababu inaburuza mkia kwenye kundi hilo, lakini ielewe pia wapinzani wao wanahitaji kulinda heshima na vile vile kuweka rekodi ya kuwachapa Wekundu wa Msimbazi nyumbani kwao.

Tunawakumbusha nyota wa Simba kushuka uwanjani wakifahamu wanapeperusha bendera ya Tanzania, hivyo wanatakiwa kujituma kwa kiwango cha juu kwa sababu pia watakuwa wanajitengenezea maisha yao kwa kuwavutia mawakala na makocha wa klabu nyingine za mataifa ya Ulaya ili kuwasajili. Huu ni wakati ambao mashabiki, wanachama na wadau wa soka nchini kuweka tofauti zao pembeni na kuiombea dua njema Simba ambayo kwenye hatua hiyo ya makundi, imepakia peke kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki.

Simba inatakiwa ifahamu si Watanzania tu wanawaangalia, mechi ya kesho itafuatiliwa na wadau wengine ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kuwavutia kuja kuwekeza kwenye soka la hapa nchini. Katika kuhakikisha mambo mazuri yanapatikana, huu ni wakati wa mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwashangilia wachezaji kuanzia dakika ya kwanza hadi pale filimbi ya mwisho itakapolia.

Mechi hiyo imepangwa kuchezwa kuanzia saa 4:00 usiku, katika kuhakikisha usalama wa mashabiki na mali zao, Jeshi la Polisi limeahidi kutoa ulinzi wa kiwango cha juu ndani na maeneo ya jirani ya uwanja huo ili kila mtazamaji atakayefika kushuhudia mchezo huo kurejea nyumbani akiwa salama.

Nipashe tunapenda kuwakumbusha wachezaji wa Simba kuepuka kufanya makosa yasiyokuwa ya lazima ili kutoigharimu timu kwa kuonyesha kadi za njano au nyekundu, na kwa kufanya hivyo, mechi hiyo itakuwa nzuri na hatimaye ndoto za kutinga hatua ya robo fainali, nusu fainali na baadaye fainali itatimia msimu huu.

Simba ikifanikiwa kusonga mbele, sio tu itajizolea mamilioni ya CAF, lakini pia itampa heshima Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele kuona wawakilishi wote wa nchi wanafanya vizuri kwenye michuano mbalimbali wanayochuana.


Katika mchezo wa soka hakuna kisichowezekana, huu ni wakati wa Simba kupambana na kushinda mechi hiyo na hatimaye kuendeleza mazuri ambayo imeyaweka katika siku za hivi karibuni, pale inapokuwa kwenye ardhi ya nyumbani.

Mungu ibariki Simba, Mungu ibariki Tanzania ambayo kesho inaingia kibaruani kusaka tiketi ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# *Coastal Union, mchagua sana huambulia koroma*

**NI** kama vile mpaka sasa Coastal Union ya jijini Tanga ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara bado haijajua tatizo linaloikabili na kuifanya timu hiyo isifanye vizuri.

Na ndiyo maana imekuwa ikitoa makocha, kuajiri wengine na baadaye kuwarudisha wale wale wa zamani.

Tayari imetangaza kumrejesha kocha wake wa zamani, Juma Mgunda. Huyu huyu ambaye ilimwondoa Agosti, mwaka jana na kumpa nafasi ya Ukurugenzi wa Ufundi, ikimwajiri Mmarekani Melis Medo kuongoza jahazi lao.

Lakini ni kocha huyu huyu Medo alitimuliwa miezi miwili iliyopita na Coastal ikawa kwenye mchakato wa kusaka kocha mwingine kwa miezi yote hii, ikiwa chini ya Joseph Lazaro, leo hii Mgunda amerudishwa tena pale pale.

Sasa najiuliza, kwa nini Coastal ilimwondoa Mgunda na sasa imeamua kumrudisha? Sababu zilizowafanya viongozi wamwondoe leo hazipo? Imetajwa ni kwa sababu timu ilikuwa inafanya vibaya, leo amebadilika nini hadi kumtegemea timu itafanya vizuri?

Je, kama timu itaendelea kufanya vibaya, itamtimua tena Mgunda? Haya ni maswali ya msingi ya kujiuliza. Na si kwa mashabiki wa Coastal Union, lakini pia kwa viongozi wao.

Zipo taarifa za ndani zinadai kulikuwa na mgawanyiko, wengine wakitaka kocha mpya, lakini wengine wakimtaka Mgunda kwa sababu ni mzoefu, anayelifahamu soka la Tanzania, mazingira ya klabu, anayeweza kufundisha kwenye mazingira hata magumu ambayo klabu inapitia, lakini kikubwa zaidi kocha ni mwanachama wa Coastal Union.

Nadhani wale waliomtaka Mgunda ameshinda kwa hoja na kusababisha arejeshwe, kwani hivi karubuni tuliwasikilia baadhi ya viongozi wakijinasibu kuwa na maombi mengi ya makocha mbalimbali wakiwamo kocha wa zamani wa Simba, Goran Copunovic, lakini Bernard Mwalala ndiye kwa kiasi kikubwa alikuwa akitajwa huenda angekuwa mrithi wa Medo. Tatizo katika klabu ya Coastal inaonekana kuwa si nani anaifundisha, ila viongozi hawajajua tatizo la msingi linaloitafuna ndiyo maana wamekuwa wakimtoa mara kwa mara Mgunda na kumrudisha.

Nionavyo Mgunda wala si tatizo klabuni hapo na ndiyo maana hata hao wanaokuja baada hali inakuwa ni ile ile.

Naweza kusema kuwa Coastal Union kwa misimu miwili imeshindwa kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kuisaidia timu baada ya kuondokewa na nyota wake mbalimbali akiwamo Bakari Mwamnyeto na Ibrahim Ame.

Katika namna ya kushangaza, bado ikamtoa kwa mkopo mchezaji, Abushehe Issa kwenda Dodoma Jiji, na kijana aliyeonekana kuwafungia mabao mengi, Hamadi Majimengi naye akitimkia Ruvu Shooting.

Ni kweli Coastal Union haijawa timu yenye uwezo wa kuwazuia wachezaji wake kuhama, hasa kwenda katika timu kubwa, lakini ikiamua inaweza kuwabakisha mastaa wake kujiunga na timu kama Ruvu Shooting, Dodoma Jiji, Biashara United au kwingineko.

Ule umoja ambao huwa unapatikana kwenye klabu hiyo kutoka kwa viongozi wa klabu, mkoa, wanachama na mashabiki wa timu hiyo wakati timu ikiwa kwenye hali mbaya ya kushuka daraja kama ungekuwepo kipindi chote, ungeweza kusababisha kupata wachezaji imara na kuzuia nyota kuondoka.

Kwa sababu ni wakati ambapo nguvu kubwa hutumika kuhakikisha timu haishuki daraja. Na hpo ndipo utakapojua kuwa tatizo la Coastal Union wala si kocha.

Niseme tu, kama viongozi wataficha sababu kuu ya Coastal kufanya vibaya na kuwa na tabia ya kutoa na kuingiza makocha na kuwarudisha tena, ipo siku mambo yatakuwa mabaya zaidi.

Waswahili wanasema kuchagua sana nazi, mwisho huchagua koroma. Kutoa makocha hakusaidii, bali ni kutafuta sababu kuu ya timu hiyo kufanya vibaya, ambayo wenyewe wanaijua nayo, pamoja na mambo mengine, ni vigisu za chinichini baina ya viongozi wenyewe kwa wenyewe, ambao huungana wanapoona timu inataka kushuka. Ipo siku watashindwa kuibakisha katika Ligi Kuu na ndipo watakapokuwa wanakumbuka shuka wakati kumekucha.

# Mama asakwa tuhuma za kumzalisha binti yake kwa kitu chenye ncha kali

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Mtaa wa Mbuyuni, Kata ya Ng'apa, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, Binti Lipongo, anasakwa na polisi baada ya kukimbia nyumba yake kwa madai ya kumzalisha mtoto wake kwa kutumia kitu chenye ncha kali na kisha kichanga kukiweka kwenye ndoo na kwenda kukitupa.

Taarifa zilizothibitishwa na ngazi ya mtaa, kata hadi mkoa, zinaeleza tukio hilo lilifanywa Februari 4, mwaka huu.

Mtendaji Mtaa wa Mbuyuni, Kitenge Selemani na Ofisa Mtendaji Kata ya Ng'apa, Maimuna Kawimba, walisema kichanga hicho kiliokotwa na wanawake wawili waliokuwa wakipitia njia eneo alikotupwa mtoto huyo kichanga.

Kawimba ambaye hata hivyo, hakutaja majina ya wanawake hao, alisema baada ya kumuokota walikwenda naye ofisi ya watendaji hao, waliokuwa kwenye kikao cha kamati ya maendeleo ya kata (WDC) kikiwa kimeviringishwa na kipande cha dera.

"Baada ya kupewa maelezo na kumuona kichanga huyo, niliongozana nao hadi zahanati na kupokelewa na muuguzi, Azizi Omari na kumpatia huduma stahiki," alisema Kawimba.

Alisema walianza msako Februari 5, mwaka huu kwa kufika nyumbani kwa Lipongo na kumkuta akiwa na binti yake ambaye hakuwa na ujauzito aliokuwa nao awali na alipohojiwa, majibu yaliwapa wasiwasi na kumchukua kwenda zahanati kufanyiwa uchunguzi wa kitaalamu.

"Wakati tukiwa kwenye mahojiano mbele ya mama yake, huyu mama alitoka nje ya nyumba yake akidai anaongea na simu na hakurejea tena," alisema Kawimba.

Mtendaji Kata huyo alisema majibu ya uchunguzi wa kitaalamu yalibaini binti huyo alikuwa ametoka kujifungua muda mfupi uliopita na walimchukua hadi Kituo cha Polisi Lindi mjini kwa ajili ya kutoa maelezo na kukabidhiwa kichanga chake kilichokuwa kimehifadhiwa kwa muda Hospitali ya Sokoine.

Muuguzi wa Zahanati ya Ng'apa, Aziza Omari, alikiri kuwapokea wateja wake hao, akiwamo kichanga chenye uzito wa kilo tatu na kumpatia huduma stahili anazotakiwa kupatiwa mtoto anapozaliwa.

Alisema siku iliyofuata alimpokea binti anayedaiwa kuwa ndiye mwenye mtoto aliyetupwa na kumfanyia uchunguzi wa kitaalamu na kubainika alikuwa ametoka kujifungua muda mfupi.

Kichanga hicho pamoja na binti huyo wamehifadhiwa Kituo cha Loving Caring Hands, kutokana na kukosa msaada wa ndugu baada ya mama yake kutoweka nyumbani kwake.

Mwandishi wa habari alipomhoji binti huyo, alidai siku ya Februari 4, 2022, mama yake alikwenda shambani, akiwa peke yake nyumbani alijisikia kwenda haja na akiwa chooni alitokwa na kitu alichodai kwa muda huo hakuweza kukitambua kama alikuwa ni mtoto.

"Niliendа ndani na baadaye nikarudi tena chooni nikakichukua kile kichanga na kwenda kukitupa porini kwani mama hakupenda nishike mimba," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Loving Caring Heart Hands, Chigogoro Mohamedi, alisema hali ya kichanga na mama yake zinaendelea vizuri na kwamba wamebeba jukumu hilo kutokana na binti kukosa msaada wa uangalizi kutoka kwa ndugu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alithibitisha ofisi yake kuwa na taarifa za aina hiyo na kueleza wanaendelea kumtafuta mama huyo ili sheria ichukue mkondo wake.

# Mrema aipongeza CCM kwa kumsamehe Membe

**Na Thobias Mwanakatwe,** KARATU

MWENYEKITI wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Augustino Mrema, amesema hatua iliyochukuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumrejeshea uanachama Bernard Membe, inaonyesha jinsi gani chama hicho kinavyoendesha siasa zake kidemokrasia.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe jana kwa simu akiwa jijini Dodoma, Mrema alisema CCM ikilinganishwa na vyama vyenzake vya ukombozi vilivyotimuliwa madarakani, imekuwa na demokrasia pana ya ndani ya chama na mifumo madhubuti ya kutatua migogoro na hivyo kuiwezesha kuhimili misukosuko.

"Ukiangalia vyama vya ukombozi katika nchi nyingine, vingi viliponzwa na ukosefu wa demokrasia na uwezo mdogo wa kushughulikia migogoro yake ya ndani," alisema.

Mrema alisema demokrasia iliyopo ndani ya CCM inapaswa kuigwa na vyama vya upinzani kwa kuwa kwa kufanya hivyo vitafika mbali kisiasa.

Katika hatua nyingine, Mrema na mke wake, Doreen Mrema, wameshiriki Mkutano Mkuu Maalum wa CCM uliofanyika jijini Dodoma baada ya kupewa mwaliko na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

"Heshima niliyopewa na Mheshimiwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa kunialika mimi na mke wangu kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, ni wa kihistoria maana viongozi wa vyama vingine wanaalikwa wao tu, sio na wake zao," alisema Mrema.

Juzi, Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM ilimsamehe na kumrudishia uanachama wake Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe.

Mwanachama mwingine aliyesamehewa na kurejeshewa uanachama wake ni Abdallah Maulid Diwani kutoka Zanzibar.

Februari 28, 2020, Kamati Kuu ya CCM chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Rais John Magufuli, ilimfuta uanachama Membe.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamidu Shaka, akizungumza na wanahabari juzi mara baada ya kikao cha NEC kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Rais Samia, alisema taratibu nyingine za kuwapatia kadi za uanachama zitafanyika katika maeneo mengine kama Katiba ya CCM inavyoelekeza.

Alipoulizwa iwapo waliwahi kuomba kusamehewa, Shaka alisema wanachama hao wamewahi kuomba kusamehewa kwa zaidi ya mara tatu ndani ya chama hicho.



Mmoja wa wafanyabiashara wa Kariakoo, jijini Dar es Salaam, Neema Mfugale, akizungumza na waandishi wa habari juzi, kuhusu mizigo yao, iliyozuiliwa katika Bandari ya Dar na kampuni ya usafirishaji ya Ghuanzhou Dingzen International Freight ya China. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Miaka 4 jela kwa wizi wa pikipiki

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu mkazi wa Kata ya Mtanda, Hassani Ally Lihami (33) kutumikia kifungo cha miaka minne gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa pikipiki yenye thamani ya Sh. 2,250,000.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Maria Betraine, baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Mshtakiwa alipotakiwa kujitetea aliomba mahakama imuonee huruma kwa madai kuwa ni kosa la kwanza kulifanya.

Vile vile, alidai kuwa ana familia akiwamo mke na watoto wanne wanaomtegemea na kwamba akipewa adhabu kubwa itakosa huduma zake.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batrane alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, iwapo ana kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hakuna. Hata hivyo, aliiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

Hakimu Batraine akitoa hukumu, alisema amesikia vilio vya pande mbili na kumhukumu kutumikia kifungo cha miaka minne gerezani na kulipa fidia ya Sh. 250,000,000.

Awali, ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Mramba, kuwa mshtakiwa alifanya wizi huo, Septemba 16, 2021 eneo la Kata ya Mkumbi, kwa kuiba pikipiki yenye namba za usajili MC 909 CMB, mali ya Ismaili Issa Omari.




Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaji Abdul Maulid, akikata utepe kuzindua maktaba ya Shule ya Sekondari ya Makumbusho, iliyokarabatiwa na Taasisi ya Read Tanzania, kwa ufadhili wa taasisi ya Karimjee Jivanjee Foundation (KJF), mkoani humo, mwishoni mwa wiki. Kutoka (kulia) ni Ofisa Mtendaji wa KJF, Caren Rowland, Mkurugenzi Mwenza wa Taasisi ya Read Tanzania, Lusekelo Mwalughelo na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Boaz Mwita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkumbo aishauri TANESCO gharama umeme

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, amelishauri Shirika la Umeme nchini (TANESCO), kuangalia uwezekano wa kushusha gharama ili wananchi waweze kutumia umeme kwa matumizi yote ya nyumbani.

Mkumbo aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ripoti iliyofanywa na Taasisi ya Afya ya Ifakara kuhusu matokeo ya tathmini ya ukuaji wa majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, ikilinganishwa na upatikanaji wa huduma za elimu na afya.

Alisema ripoti hiyo inaonyesha wananchi wanatumia umeme kwa asilimia 1.2, na Watanzania wengi hasa wa Mkoa wa Dar es Salaam matumizi ya umeme kwao ni kwa ajili ya mwanga.

Alisema inaonyesha bado gharama ya umeme ni kubwa ndiyo maana wananchi wanakimbilia kwenye matumizi ya gesi.

Mkumbo alisema TANESCO kuna haja ya kuangalia ili kushusha bei kuwawezesha wananchi wengi watumie umeme kwa matumizi mengine badala ya taa pekee. Alisema eneo jingine ni matumizi ya gesi ambayo ni asilimia 50 ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia gesi kama chanzo kikuu cha kupikia.

"Hili ni jambo kubwa kama Dar es Salaam inatumia asilimia 50 na asilimia 43 wanatumia mkaa ni jambo zuri la kupongeza kwamba wakazi wa Dar es Salaam wanatumia gesi na asilimia 1.2 wanatumia umeme hii ina maana kuwa wananchi wameona nishati ya gesi ndiyo njia sahihi ya kutumia," alisema.

Mkumbo alisema kuna umuhimu wa serikali kuongeza nguvu katika gesi kwa kuwa Watanzania wengi watatumia nishati hiyo.

"Watanzania wengi wakipatiwa nishati mbadala wanaweza kuitumia badala ya kuendelea kutumia kuni ama mkaa kwa Jiji la Dar es Salaam kutumia mkaa kwa asilimia 43 ni kubwa kuna haja ya kuliangalia tulitegemea kutumia zaidi nishati mbadala ili kulinda maeneo ya mazingira yetu," alisema. Alisema lengo la utafiti ni kupokea matokeo ya mradi wa tathmini ya hali ya maeneo endelevu katika Jiji la Dar es Salaam hasa kwa kuzingatia sekta ya afya, elimu na ukuaji wa jiji kwa ujumla.

Mkumbo alisema utafiti huo una matokeo mazuri na wameonyesha wamepiga hatua katika usambazaji wa majisafi na salama na wananchi wanapata kutoka mfumo rasmi.

Alisema kwa upande wa maji kuna jambo la kufanyia kazi kwa kuwa utafiti huo unaonyesha asilimia tano ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia mfumo rasmi wa majitaka.

Alisema walio wengi wanajihangaikia wenyewe, kuna kazi upande wa serikali na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kufanyia kazi eneo la majitaka kwa kuwa ni changamoto kubwa.

Vile vile, alisema katika ripoti hiyo imeonyesha kuna hatua kubwa ya elimu imefanywa katika uandikishwaji wa watoto shuleni kwa shule za msingi na sekondari.

Naye Msimamizi wa mradi na mtafiti kutoka Taasisi ya Afya Ifakara, Dk. Francis Levira, alisema kikubwa walichokifanya katika utafiti huo ni kupitia sera, ukuaji wa miji na kufanya sensa ya kaya.

"Tulichokikuta kuna masuala mengi ambayo tumepiga hatua kubwa kwenye usambazaji maji, kwenye elimu ya shule za msingi na sekondari kuna ufaulu mkubwa," alisema.

# KOICA kuboresha mfumo wa masomo Wete

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

NAIBU Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Korea (KOICA), Jieun Seong amesema, uboreshwaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza utasaidia kuimarisha mfumo wa elimu kwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo kazini yaliyofanyika Wete, Mkoa wa Kaskazini, Naibu huyo alisema kuwa, jukwaa hilo la viongozi watakaopewa mafunzo wanaamini litachangia kutekeleza maendeleo ya elimu nchini.

Alisema, elimu ni ufunguo wa maisha, na kwamba wanataka kuboresha masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza kwa kuweka mazingira bora ya ufundishaji, kutoa vifaa pamoja na kuwaongezea uelewa walimu na wanafunzi.

"Tunawaomba mtoe mapendekezo hapa na tunaahidi tutayafanyia kazi kwa ajili ya kujenga kwa kuwa ni miaka kadhaa tumekuwa tukishirikiana na serikali katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo," alisema.

Mkurugenzi wa mradi wa kuboresha elimu ya sekondari katika masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza (Good Neighbors), Ilsun Jung, aliishukuru Wizara ya Elimu kwa kushirikiana kuleta maendeleo na kufikia malengo ya mradi.

Akitaja baadhi ya malengo ya mradi huo, alisema ni kuijengea uwezo mifumo ya Wizara ya elimu na vituo vya elimu, ili kuwajenga walimu kutoa huduma bora kwa wanafunzi na kuboresha jamii ikiwamo kamati za shule.

Mapema akizindua mafunzo hayo, Katibu Tawala Mkoa wa Kaskazini Pemba, Ali Mohamed Mwinyi, alilishukuru Shirika hilo kwa kuleta mradi huo na tayari wameona ushirikiano uliopo baina ya Korea na Tanzania.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuitendea haki taaluma hiyo na kuwa makini wakati wanapofundishwa ili kupata uelewa zaidi kwa maslahi ya taifa.

"Ni nafasi nzuri kwetu kupata programu hizi ambazo zimetufuata nchini kwetu, kwani ingetupasa kwenda sisi jambo ambalo ingekuwa vigumu kutokana na kutomudu gharama," alisema.

Meneja mradi, Layla Ghaid alisema, wataungana na serikali kuboresha vitu vidogo na shule zisizo na vifaa zitapewa kipaumbele.

Ofisa Mwandamizi wa mradi huo, John Massenza, alisema wanataka kuboresha kiwango cha ufaulu kwa miaka mitatu ijayo, na ni vyema kusema upungufu uliopo ili wizara zipate kuwasaidia.

Akiwasilisha mada, Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji katika mradi huo, Francis Forodha, alitaja changamoto walizoziona baada ya kufanya utafiti kuwa ni uhaba wa walimu wa Sayansi, utoro na uelewa mdogo wa wanafunzi, madarasa kidogo pamoja na wanafunzi wengi kwenye darasa moja.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Sheikh Idrisa Abdulwakil Kizimbani Wete, Sabah Mussa Said na Msaidizi kituo cha Ubobezi wa Masomo ya Sayansi, Mussa Omar Khamis walisema, mafunzo hayo yatasaidia uelewa na ufaulu kwa wanafunzi, kwa kuwa walimu watafuatilia na kusomesha kwa ushindani.

Mkurugenzi Elimu ya Sekondari Zanzibar, Asya Iddi Issa, aliwataka walimu wafanye kazi kwa pamoja, wasaidiane maarifa, maelekezo pamoja na kuwa makini kwenye usajili wanafunzi ili kuepusha usumbufu wanaoupata.

Mafunzo hayo yameandaliwa kwa ushirikiano na serikali, Good Neighbors, UNOPS na NIRAS chini ya ufadhili wa KOICA ambayo yamewashirikisha maofisa elimu, maofisa taaluma na walimu wakuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

# ZAWEMA waja kujifunza vipimo WMA

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), wametembelea na kujifunza mambo mbalimbali yanayofanywa na Wakala wa Vipimo Bara (WMA).

Ujumbe wa ZAWEMA ulioongozwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban juzi ulitembelea kituo cha WMA Misugusugu Mkoa wa Pwani.

Akizungumza baada ya kutembelea kituo hicho, Waziri Shaaban alisema wamejifunza namna serikali ilivyowekeza kwenye kupima malori ya mafuta, mita za maji na mita za umeme kwenye eneo hilo.

"Tumeona mafanikio yao na namna ambavyo serikali imewekeza kwenye WMA na tumejifunza mambo mengi namna wanavyotumia teknolojia ya kisasa ambazo zingine zimetengenezwa na wataalamu wa ndani ya nchi yetu," alisema Waziri.

Alisema wanaziandaa taasisi za serikali kwenye uchumi wa buluu na ziara yao hiyo imekuwa ya mafanikio makubwa kwa kuwa wamechukua mambo mengi ambayo wataenda kufanyia kazi kwa wakala wa ZAWEMA.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema ziara hiyo ni sehemu ya kuendeleza ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Alisema taasisi hizo zinatakiwa kushirikiana kwa nia ya kuleta matokeo chanya na ZAWEMA imekuja kuona kama inaweza kutumia utaalamu unaotumiwa na WMA kujiimarisha.

"Sisi wizara tunashukuru kwa wao kuamua kuja kujifunza hapa kwa sababu wangeweza kwenda kujifunza nchi yoyote duniani masuala ya vipimo, ujio wao unaonyesha mshikamano baina ya wakala hizi mbili," alisema.

Naibu Waziri alisema Wizara ya Viwanda na Biashara iko tayari kutoa msaada wowote wa kiufundi katika kuwajengea uwezo na kuimarisha taasisi hiyo mpya ya ZAWEMA.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa, alishukuru maofisa wa taasisi hiyo kwa kutembelea WMA na kwamba itasaidia kuendelea kuimarisha uhusiano ambao tayari ulishaanza kwa muda tangu ianzishwe.

Alisema WMA imekuwa ikishirikiana na ZAWEMA tangu ianzishwe kama njia ya kuhakikisha vipimo vinavyofanyika visiwani Zanzibara na Bara vinakuwa sawa.

"Tunataka kilo moja inayopimwa Zanzibar na kilo moja inayopimwa hapa Bara iwe sawa. Kwa viongozi hawa kuja hapa ushirikiano unazidi kuimarika na tutaongea lugha moja," alisema.



## Waraibu dawa za kulevya kujengewa uwezo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuwajengea uwezo waraibu wa dawa za kulevya waliopata nafuu kwa kuwapatia mafunzo ya kukuza ujuzi kupitia vyuo vya ufundi katika fani mbalimbali ili kujiajiri na kuendelea kufanya shughuli za kiuchumi kuinua kipato chao na kuchangia pato la taifa.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Balozi Dk. Pindi Chana, alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/22 na makadirio ya bajeti ya mwaka 2022/23 ya mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya (DCEA).

Dk. Pindi alisema serikali kupitia mfuko wa dunia wa kupambana na UKIMWI, kifua kikuu na malaria (Global Fund), imepata Sh. billioni 2.4 kwa ajili ya kujenga vituo vitatu vya serikali vya kutolea huduma za utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya.

Alisema vituo hivyo vitajengwa mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Tanga.

"Kwa mwaka wa fedha 2021/22 serikali imeanzisha kliniki moja ya Methadone katika Mkoa wa Arusha na ndogo nne mkoani Dar es Salaam na kufanya jumla ya kliniki zilizopo kuwa 15 ambazo zinatoa matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya nchini na ofisi tatu za mamlaka katika mikoa ya Dodoma, Mtwara na Mwanza hivyo kupitia programu hii ya kukuza ujuzi wanufaika wa mafunzo hayo watapatiwa zana za kufanyia kazi," alisema Dk. Pindi.

Waziri Pindi alifafaua kuwa serikali inaendelea kufanya uraghibishi kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo viongozi wa kijamii, vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa dini, wanafunzi wa shule, vyuo pamoja na jamii kwa ujumla ili kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Alisema kuwa serikali imezitambua na kuzijengea uwezo asasi za kiraia 77 kwenye mikoa 18 nchini na zinafanya kazi ya kuwafuatilia waraibu na kuwaunganisha na vituo vya tiba ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambazo matumizi yake yamekuwa yakiathiri afya za watumiaji na kuharibu nguvu kazi ya taifa.

Dk. Pindi alibainisha kuwa serikali inatekeleza kampeni ya 'Furaha yangu' kwa ajili ya kuhamasisha upimaji wa VVU kwa wanaume ambayo imesaidia kuongezeka kwa idadi ya watu wanaopima VVU kutoka asilimia 61 mwaka 2016 hadi asilimia 81 mwaka 2020 wakati lengo ilikiwa ni kufikia asilimia 95 ifikapo mwaka 2023.

"Serikali inashirikiana na asasi zisizo za kiserikali na wadau mbalimbali katika upimaji na tohara kwa wanaume kupitia Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/19-2022/23," alifafanua Pindi.

Alisisitiza kuwa elimu ya lishe imetolewa kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (WAVIU) katika Konga 180 kupitia Baraza la Watu Wanaoishi na virusi vya UKIMWI (NACOPHA), kwa kuzingatia makundi matano ya vyakula ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kulima mazao yanayoweza kuwapatia chakula bora.

Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Dk. Peter Mfisi, akijibu hoja za wajumbe wa kamati hiyo, alisema kuwa mamlaka itaendelea kufuatilia matumizi ya vilevi watashirikiana na mamlaka zinazohusika.

Ili kuhakikisha wazalishaji wanazingatia afya za watumiaji huku akihimiza waraibu wa dawa hizo kujitokeza kupata matibabu waweze kurejea hali ya kawaida.

# Uwekaji anwani makazi wafikia asilimia 67

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema utekelezaji wa operesheni ya uwekaji wa anwani za makazi nchini umefikia asilimia 67.

Operesheni hiyo ilitangazwa Februari 8, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan jijini Dodoma na kuagiza uwekaji wa anwani ukamilike kabla ya kuanza kwa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu.

Nape aliyasema hayo jana kwenye mkutano na Wakuu wa mikoa nchini uliofanyika jijini hapa ambao ulilenga kutoa taarifa ya utekelezaji wa operesheni hiyo.

Alisema takwimu za mfumo unaopokea taarifa za utekelezaji wa uwekaji anwani nchini zimeonesha umefikia asilimia 67.

"Tathmini iliyofanyika ya kupata asilimia 67 imezingatia kazi zilizotekelezwa ikiwa ni kazi ya kutambua maeneo, kujenga uwezo kwa maofisa na watendaji wanaofanya kazi hii, kutoa elimu ya zoezi husika, kukusanya taarifa, kutengeneza mfumo utakaopokea taarifa na kuingiza taarifa kwenye mfumo ili ziweze kutumika na kuweka miundombinu (physical) katika maeneo mbalimbali nchini," alisema.

Alisema mwenendo wa utekelezaji unaonesha matumaini kuwa utakamilika kabla ya muda uliopangwa.

"Kazi itakayofuata itakuwa ni kusafisha baadhi ya taarifa kwenye mfumo kwa hatua za kuukabidhi kwa mujibu wa maelekezo ifikapo Mei 22, mwaka 2022," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema kazi hiyo imefanyika kwa ushirikiano mkubwa.

"Nisisitize kuwa asilimia 67 zilizofikiwa ni hatua nzuri, lakini bado tuna kazi kubwa ya kufanya, sina shaka na Wakuu wa mikoa, ujenzi wa madarasa ya mama Samia mlifanya vizuri hivyo naamini na hii operesheni ya Anwani za Makazi mtafanya vizuri," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Wakuu wa mikoa nchini, John Mongella ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, alisema operesheni hiyo inaendelea vizuri na itakamilika kwa muda uliopangwa.



Mkuu wa wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kulia), akipanda mti wa maua kwenye chungu kilichowekwa katika barabara ya Nyerere, kwa ajili ya kulipendezesha Jiji la Dodoma jana. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Jiji hilo, Dickson Kimaro. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wanafunzi 909 walioacha masomo warejea shule

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema hadi sasa takwimu zinaonesha wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali 909 wamesharudi kuendelea na masomo yao.

Naibu Waziri wa ofisi hiyo, David Silinde, aliagiza maofisa elimu watu wazima wa mikoa na halmashauri kusimamia upatikanaji wa taarifa sahihi za wanafunzi hao walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba na utoro kurudi shuleni.

Akifungua mkutano wa mafunzo elekezi kwa maofisa hao Tanzania bara, Silinde alisema wasimamizi wa elimu hiyo wanapaswa kufanya kazi kwa weledi ili wanafunzi hao waendelee na masomo.

Aidha, alisema serikali inatambua kuwa jamii iliyoelimika yenye maarifa, ujuzi na uzalendo ndiyo msingi wa maendeleo ya ujengaji wa uchumi hasa ujenzi wa uchumi wa viwanda.

"Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya watu wazima na nje ya mfumo rasmi kupitia Sera ya Elimu ya mwaka 2014 tamko namba 3.3.3. hii ni kutoa nafasi kwa waliokosa fursa katika mfumo rasmi ili kujiendeleza na kutatua changamoto za maisha au kuhitimu katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo," alisema.

"Ninawaelekeza mkafuatilie upatikanaji sahihi wa takwimu za elimu ya watu wazima na nje ya mfumo rasmi kwa kuendelea kuutumia mfumo wa BEMIS." Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, aliwataka kuendelea kusimamia na kufuatilia wanafunzi wote walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

"Mpaka sasa takwimu zinaonesha zaidi ya wanafunzi 909 wamesharudi shule kuendelea na masomo kati ya hao wapo wenye sababu mbalimbali zikiwamo utoro na ujauzito," alisema.

Alitoa wito kwa wanafunzi ambao bado hawajarudi shule kutumia fursa hiyo.

"Tunajua bado wengine wapo tumieni taratibu za kazi zenu ili kusiwe na sababu ya mtu kukosa elimu kwa kukosa fursa ambayo Rais ameitoa," alisema.

Kadhalika, Silinde aliagiza Wakurugenzi wa Halmashauri kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi na kuzisimamia utekelezaji wake.

Naye, Ofisa Elimu ya Watu Wazima Bagamoyo, Martha Ignatus, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya watumishi na kuahidi maelekezo yote wanaenda kuyafanyia kazi.



# Mtambo wa kisasa kuongoza rubani wa ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, imezindua mfumo wa mtambo wa kisasa wa kuongoza ndege katika viwanja hivyo ambayo itamuongoza rubani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya uzinduzi wa mfumo huo pamoja na kuzindua daraja la kupita abiria kwa urahisi na usalama, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Mulhat Yussuf Said, alisema kuwa mfumo huo utaongeza mapato.

Alisema kuwa viwanja hivyo vinaendelea kukua kiteknolojia na mitambo hiyo itamsaidia rubani kuongoza ndege badala ya kuwa na mfumo wa kianalogi ambao umezoeleka. Alisema kuwa mitambo hiyo itatumika katika jengo la 'terminal III' katika viwanja hivyo na utarahisisha usalama wa abiria kiwanjani hapo.

"Miongoni mwa vipaumbele vyetu mamlaka ya viwanja vya ndege ni ulinzi na usalama sasa abiria anapofika katika viwanja hivi tumezidi kukua kiusalama na tumekuwa na viwango sawa vya kimataifa," alisema.

Alisema serikali inaendelea kufanyakazi kwa kuboresha huduma muhimu kiwanjani hapo na watendaji wa mamlaka hiyo wanaendelea kutekeleza wajibu wao kwa kutoa huduma bora na kuzingatia ulinzi na usalama.

Alisema zaidi ya wafanyakazi 25 wamepatiwa mafunzo wakiwamo mainjinia na marubani kuhusu uendeshaji wa madaraja ya kupitia abiria na mtambo wa kuongoza ndege.

"Shirika la ndege linapotaka huduma hiyo tunawapatia na mashirika ya ndege yanakaribishwa na itakua miongoni mwa vyanzo vya mapato," alisema.

Kwa upande wao baadhi ya abiria waliofika kiwanjani hapo, akiwamo Jenifar Paul alisema kuwa usalama wa abiria ni mzuri na wamefurahia huduma zinazotolewa.

"Ndiyo mara yangu ya kwanza kufika Zanzibar kwa kweli nimevutiwa na mandhari nzuri ya visiwa hivi," alisema.



Baadhi ya watalii wakitembea kwenye daraja la kupita abiria katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, Zanzibar jana, wakielekea kupanda ndege ya shirila la Edelweiss kwa ajili ya safari, katika jengo la tatu jana, baada ya mamlaka ya uwanja huo, kuzindua daraja hilo pamoja na mfumo wa kisasa wa kuongoza ndege. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Rais Mwinyi awaonya wafanyabiashara kupandisha bei bidhaa Mwezi Mtukufu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewanasihi wafanyabiashara wenye tamaa kutoutumia mgogoro wa Russia na Ukraine kuwa ni kisingizio cha kupandisha bei za bidhaa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alitoa onyo hilo jana katika risala yake ya kuukaribisha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, aliyoitoa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari.

Alisema serikali haitosita kuwachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara watakaokwenda kinyume na maagizo inayoyatoa na amepata taarifa kwamba bidhaa nyingi za vyakula zitakazouzwa kwa kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani zimeingizwa nchini mapema kabla ya kuibuka kwa mgogoro wa Russia na Ukraine.

Rais Mwinyi aliwahakikishia wananchi na wafanyabiashara kwamba serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi wa dunia pamoja na gharama za kufanya biashara duniani ili kuhakikisha bei za bidhaa mbalimbali zinazouzwa kwenye maduka ya jumla na reja reja zinaakisi uhalisia wa gharama pamoja na uwezo na kipato cha wananchi.

Aliwahimiza wakuu wa taasisi zinazoshughulika na biashara, Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Masheha wahakikishe wanafuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali katika maeneo yao ya utawala na kuwachukulia hatua za kisheria wanaojaribu kukiuka sheria na maagizo yaliyotolewa na serikali.

Katika risala yake hiyo, alisema kuwa wakati Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ukikaribishwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia bado hauko katika hali ya kawaida, kama ilivyokuwa kabla ya kuzuka kwa janga la UVIKO-19, mwishoni mwa mwaka 2019.

Kadhalika, alisema pamoja na kuendelea kuwapo kwa changamoto zilizoambatana na maradhi hayo, hivi karibuni mgororo wa vita baina ya Taifa la Urusi na Taifa la Ukraine, umeibua taharuki mpya kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii duniani kote.

"Serikali zetu zote mbili zinaendelea kufatilia kwa karibu matukio hayo na kuchukua hatua za tahadhari ili kupunguza athari zinazojitokeza katika uchumi wetu," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kuwa kwa kuzingatia hali ya uchumi nchini pamoja na uchumi wa dunia kwa jumla amekuwa akiitisha vikao na watendaji wa taasisi mbalimbali za serikali kwa lengo la kujadili maendeleo ya biashara nchini na amekuwa akitoa maagizo na maelekezo yenye lengo la kudhibiti hali ya upandaji wa bei za vyakula, mafuta ya petroli na bidhaa nyingine muhimu.

Alisema kuwa kwa kipindi cha Mwezi wa Ramadhani, serikali imepunguza viwango vya kodi kwa bidhaa muhimu za vyakula na maamuzi yaliyofanywa katika suala hilo yamezingatia maslahi ya wananchi pamoja na wafanyabiashara na serikali imeweka bei elekezi kwa bidhaa muhimu za vyakula vinavyotumika zaidi katika Mwezi wa Ramadhani.

"Ni matumaini yangu kwamba wafanyabiashara wataitumia vizuri fursa hii na watahakikisha malengo ya serikali ya kuwapa wananchi unafuu wa bei za bidhaa yanafikiwa, alisisitiza Dk. Mwinyi.

Pia, alisema Mwezi wa Ramadhani umepewa hadhi na utukufu mkubwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa ni mwezi ambao umeteremshwa Qur-ani na mwezi huo imeamrishwa kufunga.

"Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutekeleza ibada ya saumu vizuri na atunufaishe na neema zote zilizoambatana na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Aliwataka Waumini kuhakikisha sadaka wanazozitoa zinawafika wanaostahili na wanaozihitaji zaidi kwa kuwa ni jambo la faraja kuona hivi sasa hapa Zanzibar zipo asasi nyingi za kiraia ambazo zinashughulikia ukusanyaji, upokeaji na ugawaji zaka na sadaka kwa wanaostahili na kurahisisha kuwatambua na kuwafika wenye kutoa pamoja na wale wenye sifa ya kupewa.

Alitoa nasaha kwa viongozi wa asasi zote zinazoshughulikia ukusanyaji na ugawaji wa zaka na sadaka zitekeleze wajibu wao kwa misingi ya upendo na uadilifu kwa kufanya hivyo watajenga imani na kuwapa nguvu zaidi wale wanaotoa mali zao kwa lengo la kutekeleza ibada hizo na kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

Alieleza kwamba ibada ya funga, kwa hakika ina mafundisho mengi ikiwa ni pamoja na kufundisha kuishi kwa pamoja, kupendana na kusaidiana.

Vilevile, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa ibada ya funga inafundisha kuwa wastahamilivu na wavumilivu, wenye subira na uwezo wa kuyadhibiti matamanio ya nafsi kwa kuwa funga ni fundisho na kigezo cha subira, jambo ambalo ni muhimu katika maisha ya mwanadamu na limehimizwa na Mwenyezi Mungu katika aya mbalimbali kwenye Qur- ani Tukufu.

# Polisi yaombwa kuwalinda waandishi wa habari kazini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Abdalla Adulrahman Mfaume, amesema Jeshi la Polisi lina wajibu wa kuhakikisha waandishi wa habari wanafanya kazi katika mazingira salama na kuhakikishiwa ulinzi.

Aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati akifungua mdahalo wa kitaaluma uliooyakutanisha makundi mawili kati ya waandishi wa habari na jeshi hilo na kujadili wajibu na majukumu yao.

Mdahalo huo uliokuwa na maudhui ya usalama kwa waandishi wa habari na uhusiano kati ya waandishi wa habari na jeshi la polisi.

Alisema wakati mwingine hujitokeza changamoto zinazosababisha pande mbili kutoaminiana hali inayopaswa kuondoka.

Alisema bado pande hizo mbili zinaendelea kushirikiana kuhakikisha jamii inapata taarifa stahiki na kwa wakati.

Mkuu wa utawala wa jeshi la polisi mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Abubakar Khatib Ally, alisema ni fursa muhimu kwa waandishi wa habari na polisi kushirikiana na kujenga uhusiano mwema katika kazi zao.

Alisema licha ya tofauti zinazojitokeza bado pande hizo mbili zinahitaji kufanya kazi kwa pamoja katika kutoa taarifa kwa wananchi. Hata hivyo, aliiomba ZPC kutumia mafunzo yanayoandaliwa na jeshi la polisi kwa askari wake kutoa mada kuhusu uhusiano mwema wa waandishi na jeshi la polisi ili ushirikiano uliopo uendelee.

Aidha, wakiwasilisha mada kwenye mdahalo huo, Mwandishi mwandamizi wa habari, Dk. Saleh Yussuf Mnemo na ASP Ramadhan Himid Haji, kutoka makao makuu ya polisi Zanzibar, walisisitiza umuhimu wa pande mbili hizo kushirikiana na kuvumiliana katika utendaji kazi wa pande hizo mbili.

Walisema kuwa licha ya kila taaluma kuwa na misingi yake, bado makundi hayo yanategemeana katika kukamilisha majukumu yao na kwambao ipo haja ya kushirikiana kikamilifu.

Walipongeza waandaaji wa mdahalo huo kwa kutoa fursa wa watendaji wa pande zote mbili kujadili kwa pamoja changamoto na mafanikio yaliyopo hatua ambayo itasaidia kufikia malengo ya kuwa na Tanzania yenye amani, utulivu na uhuru wa kujieleza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**POLISI WAVAMIA MAKAZI YA WILL SMITH**

Ukurasa.14

JUMAMOSI APRILI 2, 2022



## MWENDO WA KUKABANA

# Zuchu, Nandy sasa mguu kwa mguu

YAANI ni vita. Siyo kama ya Russia na Ukraine, hapana, ila ni ya kisanii kati ya nyota wa kike wa muziki hapa nchini.

Wasanii hao Zuchu na Nandy, ndiyo ambao wameikamata bongo fleva, kutokana na ngoma zao kuwa tamu na zinazowapagawisha mashabiki kila wanapozitambulisha tangu waanze muziki huo.

Kuanzia mwaka huu wa 2022, kila mmoja ameonekana kutaka kumuacha mwezake nyuma, lakini ni kama vile wanakabana koo. Mmoja akitoa hii, mwingine anamjibu na ile.

Tangu mwaka huu uanze, tayari kinadada hao ambao pia wana mvuto, wametoa ngoma tatu tatu ambazo zimeondokea kupendwa na mashabiki wao.

Zuchu yeye ameshatoa ngoma tatu ambazo ni I Miss You' alioimba na Rayvanny, 'Mwambieni' na 'Mtasubiri Sana' ambayo imeitoka kwa pamoja na Diamond Ptatnumz, ambazo zimeonekana kufanya vema sokoni na kujichukulia umaarufu, akionekana kama ni malkia halisi wa muziki huo kwa sasa.

Kwa upande wa Nandy ambaye yeye alianza muziki huu kabla ya wenzake, hajapoa. Anataka kumuonyesha Zuchu kuwa yeye bado mtoto ndogo kisanaa.

Ametoa ngoma ya 'Kunjani', akimshirikisha 'Sho Madjozi', nyingine aliyoitoa mwaka huu inaitwa 'Party' ambayo amemshirikisha Bill Nass, na katika kuonyesha kuwa kwenye gemu hii siyo chipukizi tena, katoa ngoma nyingine iitwayo 'Siwezi'.

BASI SAWA

## Baba Levo huo ni mkwara au...



HAIJAJULIKANA kama ni kutafuta kiki, lakini wasanii wa Bongo Fleva, Baba Levo na Shilole, ambao wamekuwa marafiki wa siku nyingi wameonekana kupeana maneno makali hadharani.

Hivi karibuni Babalevo alimuonya Shilole akae mbali na maisha yake asimfanye akaanza kuongea mambo yake.

Babalevo ameshea picha ya Shilole kwenye Insta Stori yake kwa kuandika kwamba "Kuanzia leo kaa mbali na maisha yangu mi sio hao unaowafuga nakujua vyema usitake niongee tafadhali".

## Roma ampa tano Nacha



BAADA ya mwanamuziki wa bongo fleva, Nacha kuachia kibao chake kipya "Why always me", Roma Mkatoliki ameibuka na kumwagia sifa kuwa ni kizazi cha pekee katika muziki hapa nchini.

Ngoma hiyo imezungumzia mambo mengi kuhusu maisha ya kijana wa Kitanzania ambaye anapambania maisha yake ili kutimiza ndoto zake.

"Wasanii sikuhizi wanaimba matusi tu. -wasanii sikuhizi hawaandiki vya maana,wasanii wa sikuhizi hawana tungo za kuelemisha, ebu tumfungulie milango kijana Nacha na tukipe thamani kipaji chake," ameandika.



## Hamisa unawaumiza ujue

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa kizazi kipya, Hamisa Mobeto, amezidi kuwachanganya watu kutokana na tabia yake ya kujisifu yupo katika huba zito na mpenzi wake.

Hata hivyo, safari hii Hamisa amesema yupo katika raha na mpenzi wake mpya kiasi ambacho anaweza kumsifu hadharani kuwa anampenda.

"Nipo ndani ya penzi zito, yani jamani nampenda mpenzi wangu mimi". Ameandika katika ukurasa wake wa Instagram.



## Mavoko usemayo yanatoka moyoni?

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Rich Mavoko, ametoa ya moyoni baada ya kusema yeye na Ali Kiba ni familia moja.

Hivi karibuni Mavoko ameonekana kuwa karibu na lebo ya Kings Music Records na kusababisha kuwepo na minong'ono kwamba huenda ana mpango wa kuhamia kwenye lebo hiyo.

Rich Mavoko amesisitiza kuwa atashirikiana nao kwenye masuala ya kazi, lakini kuhusu kusaini kwenye lebo hiyo haitawezekana.

## Mmh! Nandy, shikamoo mapenzi

**Na Adam Fungamwango**

TUMEUMALIZA mwezi Machi, uliokuwa na kasheshe nyingi kwenye tasnia ya sanaa, kwenye bongo fleva, bongo muvi, muziki wa dansi, hip hop, taarabu na mingine.

Na hii ilitokana na sekeseke la Steven Mengere, maarufu kama Steve Nyerere na Shirikisho la Muziki Nchini Tanzania.

Imeandikwa sana wiki iliyopita, hivyo haina haja ya kurudia. Kwa sasa tumeuanza mwezi Aprili. Sijui utakuwa na yapi tena. Mbali na timbwili hilo, haikuwazuia wasanii kutoa ngoma zao. Tumeshuhudia wasanii wakubwa nchini wakitakata kwa ngoma kali mwezi Machi.

**SIWEZI-NANDY**

Msanii maarufu wa kike, Nandy, yeye mwezi Machi ametisha kwa kutoa pini moja kali aliloliita 'Siwezi'.

Ni wimbo wa mapenzi, alilalamika kuachwa "kumbe kuachwa kunauma hivi? Mapenzi shikamoo, sirudii tena, umepatwa na nini, si useme kinachokufanya uniteme?" Ni moja kati ya mashairi yaliyomo kwenye ngoma hiyo ambayo imetoka Machi 23.

Kuna kipande cha video kwenye ngoma hiyo ndiyo kimekuwa gumzo, kwani anaonekana msanii huyo akiwa ndani ya sanduku la kuzikia.

**FINE-DIAMOND PLATNUMZ**

Diamond naye hakupoa. Yeye akatoka na ngoma 'Fine' mwezi Machi. Ameitoa Machi 24, siku moja tu baada Nandy kutoa ngoma yake. Kwenye video ya wimbo huo, Diamond ameonekana akiwa kwenye mavazi ya kijeshi.

**UMENIWEZA-OMMY DIMPOZ**

Machi 18, msanii mkongwe wa bongo fleva Ommy Dimpoz yeye akatoa ngoma yake iitwayo 'Umeniweza' na kuwa mmoja wa wasanii ambao hawakuupitisha mwezi huo hivi hivi.

**LEMMY-BEST NASO**


Ni kisa cha kusikitisha cha dereva wa daladala kumfumania mkewe kwa kijana mmoja wa mtaani. Lakini hakumfanya chochote, akamchukua mke wake na kurudi naye nyumbani.

Kutofanya chochote, wala kuonekana kuchukizwa na tukio hilo kulikuwa ni kama kisu kwenye moyo mke wa dereva wa daladala, kwani siku zote akawa anafikiria mumewe atafanya nini? Anafikiria nini? Mbona hajamuadhibu? Lemmy, ambaye ndiye mke wa dereva huyo wa daladala, anaamua kuomba talaka, mume hataki hilo litokee, badala yake anampa upendo wa hali ya juu. Mke bado haamini anataka kutoroka. Machi 31 ndiyo imetoka ngoma hii ya Best Naso.

**BAKHRESA-HARMONIZE**

Harmonize, Machi 20 alitoa ngoma yake, akaamua kuiita 'Bakhresa'. Naye akaingia kwenye orodha ya wasanii ambao wametoa ngoma zao mwezi Machi. Mwezi uliokuwa na pilika pilika nyingi upande wa wasanii.






## Nani Shujaa?; Umemshinda baba, si mtoto

**Na Adam Fungamwango**

WALE waliosema kuwa malipo ni hapa hapa ulimwenguni, wajengewe sanamu. Ni kwamba mara nyingi sana yoyote anayefanya maovu, Mungu huamua kumuadhibu hapa hapa ulimwenguni. Ni mara chache sana kusubiri kwenda kulipiwa mbinguni.

Ukitapeli na wewe utatapeliwa, ukiiba na wewe utaibiwa na hata ukiua na wewe utauawa. Halafu kuua ni mbaya sana kwa sababu unaweza kuuawa siku ambayo hutegemei na hata anayefanya hivyo utabaki unashangaa. Na ndipo utakapoamini kuwa damu nzito kuliko maji.

Hebu leo tuiangalie filamu iitwayo 'Nani Shujaa', imechezwa na kina Emaely Daud, Athumani Chalamanda, Omari Lyombam Sanastian Mwanangulo na wengine wengi.

Inaanza kwa kuonyesha mtu mmoja wa makamu anavamiwa na majambazi na kuuawa. Yule mtu alikuwa na familia yake ya watoto wawili wa kike na wa kiume, na mke. Yeye na mkewe wanauawa na majambazi lengo lao ilikuwa ni kuchukua pesa. Waliporidhika na pesa wakaondoka.

Watoto wa marehemu wanasambaratika kila mmoja akienda kivyake.

Mtoto wa kiume akaanza kazi ya kuokota makopo, baadaye akaosha magari. Siku moja akakorofishana na tajiri yake wakati anaosha gari la jamaa mmoja. Yule jamaa akamchukua mtoto na kuamua kumsaidia kumpeleka akafanye kazi zingine. Huyo mtoto anaitwa Dame.

Kumbe alichukuliwa na mmoja wa watu walio kwenye kundi la wauza madawa ya kulevya. Akampeleka kwa bosi wake Mr Paul. Akamfundisha ngumi na kila aina ya mapigano. Lengo ni kupambana na yeyote atakayeonekana kutaka kuwaharibia kazi.

Upande wa pili ni ofisa wa polisi Tonny anayepambana na wauza madawa ya kulevya. Anakutana na binti mmoja anaitwa Jacky, anampenda na kukaa naye. Lakini siku moja wanakorofishana, Jacky anaondoka. Anarudia kazi yake za zamani ambayo ni kujiuza. Akiwa na wenzake inakuja gari na kuwachukua. Kumbe ni wauza madawa ambao waliwachukua wasichana hao kwa kuwateka, lengo ni kuwasaidia kufunga unga kwenye mifuko. Mateso wanayoyapata, wanamuumiza Dame, hasa msichana Jacky. Aliondokea kupenda. Baadaye akagundua kuwa ni dada yake ambaye walipotezana naye baada ya baba yao kuuawa. Mle ndani kwenye jengo hilo, Dame pia alizifuma picha zilizoonyesha baba yake akipigwa risasi. Ndipo alipogundua kuwa kundi lake hilo ndilo lililomuua baba yake. Analigeuka na kuanza kupigana nalo kwa lengo la kulipiza kisasi, pia akitaka kujiokoa yeye na dada yake. Kupambana na kundi hili hatari ni kazi ngumu. Afande Tonny naye akafika hapo na vijana wake baada ya kuletewa habari kuwa kuna kundi la wauza madawa.

# Polisi wavamia makazi ya Will Smith



POLISI katika jiji la Los Angeles, wamevamia nyumba ya mwigizaji na mwanamuziki Will Smith, baada ya siku chache kumzaba vibao mchekeshaji Chris Rock katika tuzo za Oscar.

Rock alimfanyia utani mke wa Smith, Jada kutokana na mtindo wa nywele zake kuwa umeficha ugonjwa jambo ambalo lilimkera msanii huyo.

Maofisa hao wa polisi walifika katika jumba la Smith, linalofahamika kama Calabasas mansion na kuanza kufanya uchunguzi pamoja na kuchukua picha kadhaa ambazo zinadaiwa zitatumika katika kutafuta ushahidi.



## Anthony, Alvina wapeana talaka

MSANII wa filamu kutoka Hollywood, Anthony Anderson na mkewe Alvina Stewart, ndoa yao imefikia ukingoni baada ya kuishi kama mume na mke kwa miaka 22.

Alvina ndiye ameamua kuomba talaka katika mahakama ya Los Angeles, akieleza mume wake hana uaminifu kutokana na kutoka kimapenzi na wanawake tofauti.

Awali Alvina alifungua kesi kama hiyo mwaka 2015, lakini aliamua kuiondoa mahakamani baada ya kupata suluhu wao wenyewe.

## Baldwin hataki uzazi wa mpango

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Marekani, Alec Baldwin anatarajia kupata mtoto wake wa saba na mkewe Hilaria Baldwin.

Kuwa na idadi kubwa ya watoto ni jambo gumu kwa familia za Marekani, lakini kwa Hilaria na mume wake suala hilo haliwasumbui na wanataka kuongeza zaidi ya walionao sasa.

"Baada ya kupanda na kushuka miaka michache iliyopita, tunafurahi kuwapa mshtuko kwa kuwaletea Baldwin ambaye anakuja hivi karibuni," ameandika Hilaria.





## Lil Frosh hii ni bahati yako

SHTAKA la unyanyasaji wa kijinsia lilomkabili nyota wa muziki nchini Nigeria, Lil Frosh, hatimaye limefutwa baada ya mlalamikaji Sanni Goriola, kuamua kutoendelea na kesi hiyo.

Lil Frosh alikamatwa mwaka 2020 akituhumiwa kumpiga mwanamke huyo ambaye alikuwa mpenzi wake na kumsababishia majeraha makubwa usoni.

"Napenda kuwashukuru kila mmoja aliyesimama upande wangu kutokana na kupigwa na Lil Frosh, na pia nataka kuwaeleza kesi yetu nimeiondoa mahakamani," ameandika Sanni.

## Mr Ibu kweli walitaka kukumaliza?

STAA wa filamu kutoka Nollywood, John Okafor, ambaye anajulikana kama Mr Ibu, ameibua kashfa nzito baada ya kudai aliwekewa sumu katika tukio moja mjini Abuja.

Msanii huyo mkongwe amesema alilazwa hospitali kwa siku kadhaa kutokana na hali yake kuwa mbaya.

"Nimepewa sumu tena, nawaona maadui zangu wananitumia kuonyesha nguvu zao. Mara hii sikupewa sumu kijijini, nimepewa mjini Abuja," aliandika Mr. Ibu.



MAKALA

UTAFITI MPYA WAONYESHA

# Chembe za plastiki zagundulika kwenye damu ya binadamu



Chembechembe za plastiki zilizogundulika kuwa kwenye damu ya binadamu

**Mwandishi Wetu**

UCHAFU unaosababishwa na chembe za plastiki umegundulika kwa mara ya kwanza kwenye damu ya binadamu, baada ya wanasayansi kukuta chembe kwenye takriban asilimia 80 ya watu waliofanyiwa uchunguzi.

Ugunduzi unaonyesha chembe hizo za plastiki zinaweza kusafiri mwili mzima na zinaweza kukaa kwenye ogani.

Athari zake kwa afya bado hazijajulikana, lakini watafiti wanasema chembe za plastiki husababisha madhara kwenye seli za binadamu na chembe chafu za hewa zinajulikana tayari kuingia mwilini na kusababisha mamilioni ya vifo vya mapema kwa mwaka.

Kiasi kikubwa cha plastiki isiyofaa kinatupwa ovyo kwenye mazingira wanayoishi watu na chembe hizo za plastiki sasa zinachafua sayari nzima, kutoka kilele cha Mlima Everest hadi kwenye vilindi vya bahari .

Watu wanaojulikana tayari kuwa na chembe za aina hii, wamepata kwa njia ya chakula, maji na kuvuta pumzi. Pia zimegundulika kwenye kinyesi cha watoto na watu wazima.

Wanasayansi walichunguza sampuli za damu kutoka watu 22, waliojitolea kutoa damu na kugundua chembe za plastiki kwenye sampuli za damu za watu 17.

Nusu ya sampuli zilikuwa na aina ya plastiki inayotumika kutengeneza chupa za vinywaji (yaani 'plythylene terephtahalate' au kwa kifupi (PET), wakati theluthi mbili ya sampuli zilikuwa na aina ya plastiki inayotumika kutengeneza vifungashio vya vyakula na bidhaa zingine.

Robo ya sampuli za damu ziligundulika kuwa aina ya plastiki iitwayo 'polyethylene', ambayo hutumiwa kutengeneza mifuko ya plastiki.

"Utafiti wetu ni dalili ya kwanza kwamba tuna chembe za plastiki kwenye damu yetu ni matokeo mapya," alisema Profesa Dick Vethaak, mtaalamu wa elimu juu ya asili na athari za sumu kwenye ikolojia, Chuo Kikuu cha Vrije Amsterdam, Uholanzi.

"Lakini hatuna budi kupanua wigo wa utafiti na kuongeza ukubwa wa sampuli na idadi ya chembe za plastiki ambazo zitachunguzwa, utafiti zaidi unaofanywa na watafiti mbalimbali tayari unaendelea," anasema.

"Ni jambo la maana kuguswa na hali hii," Vethaak aliliambia gazeti la The Guardian la Uingereza. "Chembe za plastiki zipo na zinasafirishwa mwili mzima," aliongeza.

Anasema utafiti wa awali ulionyesha kwamba chembe za plastiki zilikuwa mara 10 zaidi kwenye kinyesi cha watoto, ukilinganisha na cha watu wazima na kwamba watoto wanaolishwa kwa chupa za plastiki wanameza mamilioni ya chembe za plastiki kwa siku.

"Tunajua pia kwa jumla watoto wachanga na wadogo wako hatarini zaidi kwa kemikali zitokanazo na chembe za plastiki, jambo hili linanipa wasiwasi sana," anasema.

Utafiti mpya umechapishwa kwenye jarida liitwalo 'Environment International' na limetumia mbinu zilizopo kugundua na kuchunguza chembe za plastiki zenye ukubwa unaofikia milimeta zipatazo 0.0007.

Baadhi ya sampuli za damu zina aina mbili au tatu za plastiki. Timu ya watafiti ilitumia sindano zinazotumia sirinji za chuma na neli za kioo kuepuka uchafu na kupima viwango vya chembe za plastiki kwa kutumia sampuli zilizoandaliwa.

Vethaak anakiri kwamba kiasi na aina za plastiki zilitofautiana kwa kiasi kikubwa kati ya sampuli za damu, huku akiongeza kwamba huu ni utafiti unaoongoza.

Anasema kwamba tofauti zinaweza kuakisi kuwa kwenye chembe za plastiki kwa muda mfupi kabla ya sampuli za damu kuchukuliwa, kama vile kunywa kahawa kwa kutumia kikombe cha plastiki, au kuvaa barakoa iliyotengenezwa kwa plastiki.

"Maswali ni nini kinatokea mwilini mwetu?", Je, chembe za plastiki zinabaki mwilini? Zinasafirishwa kwa baadhi ya ogani? Na viwango hivi vinaweza kusababisha maradhi? Vathaak anajibu kwamba inahitajika haraka kufanya utafiti zaidi ili kuweza kujua ni nini kinachotokea.

Utafiti huu mpya ulifadhiliwa na Shirika la Taifa la Uholanzi linaloshughulikia utafiti wa Afya na Maendeleo na Bahari ya Pamoja, linalofanyakazi ya kupunguza uchafu wa plastiki.

"Uzalishaji wa plastiki unakadiriwa kuongezeka mara dufu ifikapo mwaka 2040," anasema Jo Royle, mwanzilishi wa shirika lijulikanalo kama 'Charity Common Seas'.

"Tuna haki kujua plastiki yote hii inafanya nini kwenye miili yetu," anaongeza

Shirika la 'Common Seas', pamoja na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali zaidi ya 80, wanasayansi na wabunge, wameiomba serikali ya Uingereza kutenga paundi milioni 15 kwa ajili ya utafiti juu ya athari za plastiki kwa afya ya binadamu.

Jumuiya ya Umoja wa Ulaya tayari inafadhili utafiti juu ya athari za chembe za plastiki kwa vijusi na watoto wachanga, na juu ya mfumo wa kinga na maradhi.


Utafiti wa hivi karibuni umegundua kwamba chembe za plastiki zinaweza kukaa kwenye utando wa nje wa seli nyekundu za damu na zinaweza kuzuia uwezo wake wa kusambaza hewa ya oksijeni.

Chembe hizi pia zimegundulika kwenye kondo la nyuma la wanawake wajawazito na kwenye panya wenye mimba zinapita kwa haraka kupitia mapafu kwenda kwenye moyo, ubongo na ogani zingine za vijusi.

Gazeti jipya la mapitio linachochapishwa kila Jumanne, lililoandikwa kwa pamoja na Vethaak, lilichunguza hatari ya saratani na kuhitimisha.

"Utafiti wa kina zaidi kuhusu jinsi chembe chini ya milimeta tano na chini ya nanometa 100 zinaathiri miundo na mifumo ya mwili wa binadamu, na kama kwa jinsi gani zinaweza kubadilisha seli na kusababisha saratani, hasa kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa plastiki.

"Tatizo linakua kwa haraka zaidi kila siku," alitahadharisha.



Baadhi ya vyombo vya plastiki vinavyosadikika kuchangia tatizo hilo

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOELEKEA...

# Michezo ya watoto iliyopotea

## •Goroli, mdako, 'kujipikilisha'
## •Kombolela,sarakasi nayo imo

Na Adam Fungamwango

KULIKUWA na michezo mingi sana enzi hizo, hasa kwa watoto na vijana.

Ukiangalia zamani na sasa, utagundua kuwa watoto na vijana wa miaka ya nyuma walikuwa wanacheza michezo mingi iliyosababisha kuwa imara kiafya, pamoja na utimamu wa mwili.

Leo tunaangalia michezo ya watoto kuanzia miaka ya nyuma hadi katikati ya miaka ya 1990, ilipoisha nguvu. Tunaanza na michezo ya watoto wa kike.

Kwanza kabisa kulikuwa mchezo wa kipande. Huo ulichezwa kwa kuchora kwenye ardhi mistari mingi mfano wa boksi. Sehemu moja ya boksi ilikuwa tupu na nyingine imekatwa kati na mstari mwingine.

Mchezaji anatakiwa kukanyaga mguu mmoja kwenye boksi ambalo liko tupu na miguu miwili boksi ambalo katikati litakuwa limepigwa msitari.

**MCHEZO MWINGINE MAARUFU NI 'REDE'.**

Wanawake, kuanzia watoto wa miaka mitano, saba na kuendelea wakati mwingine hata mpaka miaka 25, walikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza mchezo huo.

Ulichezwa kwa mmoja kukaa upande huu na mwingine upande wa pili, mmoja akiwa kati. Hawa wa pembeni wanakuwa na mpira mmoja, kazi yao ni kurusha ili kumbabau au kumpiga yule wa kati.

Wa kati kazi yake kubwa ni kukwepa mpira ambao wenzake wanawania kumbabua nao. Burudani ya mchezo huo kwa waangaliaji ipo zaidi kwa yule wa kati, kwani walikuwa na staili mbalimbali za kuukwepa mpira huo, ambao ndiyo unaosisimua na kuchangamsha mchezo mzima.

Ataruka juu mpira upite kati. Atanyumbulika kama mcheza sarakasi, atainama, atapiga magoti, au kuanguka chini, ili mradi tu mpira usimpige.

Kujipikilisha pia ni mchezo wa watoto wa kike ambao walikuwa wakiigiza mama zao kupika. Kuna wadogo zaidi waliopika kwa kutumia michanga, makopo, au sufuria ndogo na moto wanaochukua kutoka kwa mama zao.

Wakati mwingine wanachezea mwanasesere, na vitambaa, wanajenga nyumba kwa kutumia michanga na udongo, huku wakiigiza kama wao ndiyo mama wenye nyumba na wanasesere ni watoto. Basi watawaogesha na kuwavisha nguo nzuri kama binadamu, na hata kuwakaripia, wakiiga yale yale yanayofanywa na mama zao, kwao.

Kulikuwa na michezo ya kuruka kwamba. Yote hiyo ni kwa watoto wa kike.



**Michezo mingine ya wavulana ni goroli na kutengeneza magari kwa kutumia mabua ya miti mbalimbali kwa wale wa vijijini, lakini kwa mijini watoto walitumia sana maboksi na makopo.**

Michezo ya kiume kwanza kabisa ilikuwa ni mpira wa miguu, sarakasi, na kuna michezo hatari ya kujivingirisha katikati ya gurudumu, huku watoto wengine wakiwa wanaliendesha.

Michezo mingine ya hatari ambayo hii ilikuwa ikikatazwa na wazazi, lakini watoto walikuwa wafanya kwa uficho ni kudandia magari.

Kombolela ni mchezo mwingine ambao wengine wanakwenda kujificha, mmoja anakuwa analinda chupa moja ya plastiki isipigwe teke na yeyote aliyekuwa amejificha.

Kanuni ni kwamba wa kwanza kutajwa ndiye anayelinda au kusafa kama lugha ya mchezo inavyosema.

Msafaji atamtaja mmoja mmoja atayejitokeza kwa lengo la kutaka kubutua, au kupiga teke chupa ile kabla hajaifukia. Chupa ikipigwa teke kabla hajataja jina, basi wote waliotajwa watarudi tena kujificha na yeye ataendelea na kazi ile ile, hadi atakapofanikiwa kutaja wote. Hii inamfanya msafaji awe makini mno. Huu ni mchezo wa watoto wa jinsia zote.

Michezo mingine ya watoto wavulana kwa wasichana ni 'tayari bado', kucheza kwenye mvua, ukuti ukuti, kioo alikivunja nani, na hata kula mbakishie baba, ambao mtu akiangusha kijiti, anachezea kichapo hadi aende kushika kitu walichoahidiana kama mtu, nyumba, au chochote kile ambacho ukikifikia na kukishika umeua adhabu ya kupigwa kwa kosa la kuangusha kijiti.

Michezo mingine ya wavulana ni goroli na kutengeneza magari kwa kutumia mabua ya miti mbalimbali kwa wale wa vijijini, lakini kwa mijini watoto walitumia sana maboksi na makopo.

Kuendesha magurudumu ya gari, pikipiki, basikeli, au ringi, na hii iliwafanya watoto kupendwa kutumwa na mtu yoyote yule wa jirani, si lazima awe mzazi wake, ili aende dukani au sehemu yoyote ile mbali, apate nafasi ya kuendesha au kusukuma gurudumu lake.

Pia kulikuwa na mchezo wa watoto kuchukua mbwa na kwenda kuwinda. Kwao ulikuwa ni kama mchezo na ilikuwa ni kama furaha tu kwao kufanya hivyo na wala hawakuwa wanaichukulia kama ni lazima warudi na mnyama. Ilikuwa ni kama mtoko tu. Na hata wanachokwenda kuwinda ni ndezi, sungura. Wakati mwingine wanarudi nao, wakati mwingine hawaambulii chochote, lakini wanakuwa wamechoka na kuchafuka, huku mioyo yao ikiwa imeridhika na shughuli walioifanya.

Inayofanana na hiyo ni ile ya kwenda kukamata wadudu kama panzi wa aina mbalimbali kama baranguru, au 'balale' kama walivyokuwa wakiita wenyewe.

Hiyo na mingine mingi ndiyo ilikuwa michezo ya watoto wa zamani ambayo iliwaweka 'bize' kweli kweli kiasi cha kuwa hawakutegemea akili za shuleni tu kwenye maisha yao, lakini pia kuwa na elimu ya kujitegemea kwani waliweza kufanya, kutengeneza au kuwa na ujasiri wa kufanya kitu chochote kikubwa chini ya umri wao, kiasi cha kuweza hata kuanza kuondoka kwa wazazi wao wakienda mbali kutafuta maisha na kujitegemea wenyewe wakiwa kwenye umri mdogo, bila kuwa tegemezi kwa wazazi wao kwa muda mrefu.



**Tuma meseji 0716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

## Wanajeshi wa Russia wapora magari ya raia

**KYIV,** UKRAINE

VIKOSI vya Ukraine vinasema kuwa zoezi la kuondolewa kwa sehemu ya vikosi vya Russia kutoka Kaskazini mwa Kyiv, kuelekea mpaka na Belarus, bado linaendelea.

Taarifa ilisema kwamba kulionekana safu kubwa ya magari ya kijeshi na ya kiraia pamoja na mabasi, malori na magari madogo ambayo yaliibwa na vikosi vya Russia.

Vikosi vya Russia pia vilichukua mali zilizoibwa katika maeneo mengine ambayo yalikuwa yanakaliwa na wanajeshi hao.

Vikosi vya Ukraine viliharibu vifaru vitatu, magari mawili ya kivita, magari mawili na mifumo miwili ya kukabiliana na makombora.

## Russia yaishutumu Ukraine kushambulia ghala

**MOSCOW,** RUSSIA

GAVANA wa jimbo la Belgorod nchini Russia, ameishutumu Ukraine kwa kushambulia ghala lake la mafuta katika mji huo.

Vyacheslav Gladkov alisema kupitia Telegram kwamba moto mkubwa uliozuka Ijumaa asubuhi kwenye ghala hilo, ulisababishwa na mashambulizi ya anga kutoka kwa helikopta mbili za Ukraine.

Awali alisema kuwa watu wawili walijeruhiwa, lakini hakukuwa na hatari yoyote ya kutishia maisha. Wakazi wa mitaa ya karibu waliondolewa wakati maofisa wa zima moto wakikabiliana na moto huo, alisema.

Hatua hiyo inajiri siku mbili tu baada ya eneo hilo pia kushuhudia milipuko mwingine katika jengo la kuhifadhia silaha. Belgorod iko kaskazini mwa mpaka wa Ukraine.

Ukraine haijathibitisha kuhusika na milipuko au mashambulizi hayo.

**DW**

## Wataalamu Msumbiji kuchunguza mtu kufufuka

**MAPUTO,** MSUMBIJI

KIJANA mmoja Kaskazini mwa Msumbiji ambaye alidhaniwa kufariki dunia na mazishi yake yalifanyika mwezi Novemba mwaka jana, amekutwa akiwa kijijini kwao Lindi.

Jumuiya inamtaja Eurelia Manuel Benjamim, kama mtu aliyefufuka kutoka kwa wafu, lakini alisema alikuwa ameenda tu kufanya kazi katika shamba la mjomba wake kwa miezi michache.

Msimamizi wa eneo katika wilaya ya Montepuez alimueleza mtangazaji wa serikali kuwa walifanya sherehe zote za mazishi ya siku ya tatu na kutembelea kaburi ambalo halijavunjwa.

Kikosi cha wataalamu kinatumwa Lindi kufanya uchunguzi ili kuona ni nani au nini kilizikwa kaburini.

**BBC**

# Msalaba Mwekundu kujaribu kuingia Mariupol

**KYIV,** UKRAINE

MSAFARA mdogo wa Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) wa magari matatu pekee, umeondoka Zaporizhzhia kuelekea Mariupol kwa lengo la kujaribu kuhamisha raia waliokwama kutoka katika mji huo uliozingirwa.

Timu ilipokea dhamana za usalama zinazohitajika mapema.

Waokoaji hao wanataka kufanya operesheni ya siku moja, wakitarajia kukutana na mabasi kwa ajili ya kuwahamisha watu zaidi.

Msaidizi wa Meya wa Mariupol, alisema jiji hilo la Kusini mwa Ukraine, lililozingirwa lilisalia kufungwa kwa yeyote anayejaribu kuingia na likikuwa hatari kwa yeyote anayejaribu kuondoka, shirika la habari la Reuters linaripoti.

Petro Andryuschenko, alisema vikosi vya Russia vimekuwa vikizuia vifaa vya kibinadamu kuwafikia wakazi walionaswa, na kuweka wazi kuwa ukanda wa kutoa misaada ya kibinadamu uliopangwa haujafunguliwa.

**BBC**



Mwanajeshi wa Ukraine akiwa na mbwa akiwa ndani ya nyumba iliyoteketezwa kwa mabomu wakati akipambana na vikosi vya Russia katika mji wa Irpin. **PICHA: THE NEW YORK TIMES**

# Miili zaidi ya watoto yapatikana

**ABUJA,** NIGERIA

MIILI mingine mitano ya wahanga wa ajali ya boti imepatikana baada ya kazi ngumu ya uokoaji inayoendelea kwa siku ya tatu.

Ajali hiyo ilihusisha wanawake na watoto wanaokimbia magenge yenye silaha katikati mwa Nigeria.

Mkuu wa shirika la dharura katika jimbo la Niger, Ahmad Ibrahim Inga, aliiambia BBC kuwa miili ya watoto wanne na mtu mmoja ilipatikana siku ya Alhamisi.

Mpaka sasa jumla ya watu 13 wamethibitishwa kufariki katika ajali hiyo ya boti- 10 kati yao wakiwa ni watoto na wote wameshazikwa.

Waathiriwa walikuwa wakikimbia shambulio la bomu katika kijiji cha Galkogo katika jimbo la Niger siku ya Jumanne. Boti yao ilizama kwenye mto mkubwa.

Maofisa walisema boti iliyobeba watu kadhaa ilikuwa dhaifu na ilikuwa imejaa kupita kiasi.

Magenge yenye silaha nchini humo yameongeza mashambulizi kaskazini mwa Nigeria na kuwatawanya karibu watu milioni moja.

**BBC**

# Wanne wafa kwenye ajali ya ndege

**SEOUL,** KOREA KUSINI

NDEGE mbili za Korea Kusini zimegongana angani wakati wa mazoezi na kuanguka karibu na kambi yake na kuua watu wote wanne waliokuwamo ndani yake.

Kulingana na mamlaka ya kijeshi, ndege hizo za mafunzo chapa KT-1 zilianguka karibu na mji wa Sacheon, takriban kilomita 300 kusini mwa mji mkuu Seoul.

Ajali ya jana ndiyo tukio la karibuni zaidi linalohusisha ndege za jeshi la anga la Korea Kusini kwa mwaka huu.

Mnamo mwezi Januari, rubani wa jeshi la anga alikufa katika ajali ya ndege ya kivita ya F-5.

Tukio hilo lilitokea muda mfupi baada ya taifa hilo kusimamisha matumizi ya ndege zake zote za kisasa za F-35, baada ya mojawapo kutua kwa dharura kutokana na kasoro za kimfumo.

**DW**

# Kodi sekta ya ujenzi kichocheo ukuaji uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

ULIPAJI kodi kwa kuzingatia miongozo kutoka kwa wadau na wataalam wa sekta ya ujenzi ni miongoni mwa vichocheo vya ukuaji wa uchumi hali itakayopunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.

Kaimu Katibu Mkuu, Richard Mkumbo, alisema hayo wakati akifungua mafunzo endelevu ya Wataalam wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kwa niaba ya katibu Mkuu wa sekta hiyo jana Jijini Dodoma na kusisitiza pamoja na kodi hizo serikali inawekeza nguvu katika ushirikishwaji wa sekta binafsi ili kukuza sekta hiyo.

Mkumbo alisema kikao hicho kitajikita katika masuala yanayojitokeza kwenye Sheria ya Kodi hususani katika sekta ya ujenzi, malipo ya kodi kwa njia ya kielektroniki na kujaza fomu za ushuru zitakazowasilishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Kwa siku mbili hizi kupitia mafunzo haya, nina imani tutatoka hapa na michango itakayosogeza sekta ya ujenzi mbele na lengo ni kuhakikisha kuwa kasi ya utekelezaji wa miradi inabadilika kwa kasi kubwa," alisema Katibu Mkuu Mkumbo.

Kadhalika katika suala la kuvutia uwekezaji na kudhibiti kodi za serikali sekta ya ujenzi, serikali inaendelea kuhakikisha kuwa inafanya maboresho hususani kwenye eneo la misamaha ya Kodi la Ongezeko la Thamani (VAT)

Aidha, Mkumbo aliwasihi wataalam wote kuzingatia na kutoa kipaumbele kwa Sheria na Kanuni za Kodi wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kuwa shughuli za ujenzi zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi.

Alisema, kwa mujibu wa taarifa ya ukuaji 2020, shughuli za ujenzi zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi kwa asilimia 27.5, zikifuatiwa na kilimo kwa asilimia 25.8, usafiri na uhifadhi asilimia 13.6 na shughuli za uzalishaji viwandani asilimia 7.8.

Awali akiwasilisha taarifa ya Bodi Mbunifu Majengo Edwin Nnunduma, alisema kuwa toka mwaka 2003 Bodi imejipangia ratiba za kuendesha Semina za Mafunzo Endelevu (Continuing Professional Development (CPD) kwa lengo la kuwanoa wataalam waliosajiliwa na Bodi ili kuwawezesha kuendana na maendeleo au mabadiliko ya Sheria, Kanuni, Sayansi na Teknolojia yanayotokea ulimwenguni.

Alisema mada zitakazowasilishwa zina lengo la kuwakumbusha Wataalam hao umuhimu wa kufuata na kuzingatia maadili na utawala bora katika ulipaji wa kodi za serikali.

Mbunifu Majengo, Edwin Nnunduma, alisema kuwa Bodi imefanikiwa kuboresha utaratibu wa kusajili wataalam na miradi kwa kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Bodi ujulikanao 'Online Registration System (ORS) ambao utasaidia wataalam wanaotaka kujisajili au kusajili miradi wanawasilisha nyaraka zao kwa njia ya mifumo ya mitandao bila kufika kwenye ofisi za Bodi.

"Maboresho yaliyofanyika katika mfumo huu ni rahisi na wa Kisasa, kwani humuwezesha Mtaalam kuwasilisha nyaraka akiwa mahala popote ambapo anaweza kupata huduma za mtandao" amesema Nnunduma.

Kufikia Februari, 2022 Bodi imesajili wataalam 1,377 na kusajili kampuni za kitaalam 486. Wataalamu 132 na kampuni 72 wamefutiwa usajili kutokana na makosa mbalimbali.

Mafunzo hayo ya siku mbili yamefanyika jijini Dodoma kwa kuwakutanisha wataalam zaidi ya 300 kupata uzoefu, kujadili na kutafuta suluhu za changamoto mbalimbali zinazowakuta.



Baadhi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi kutoka mikoa mbalimbali wakimsikiliza mgeni rasmi Kaimu Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi, Richard Mkumbo, (Hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wataalam hao, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machali ahamasisha utunzaji miti makazi ya watu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera, Moses Machali, ameitaka idara ya mazingira kutengeneza ratiba na wenyeviti wa mitaa na vijiji ili kuwawezesha kutunza miti inayopandwa karibu na makazi yao.

Machali alitoa kauli hiyo wakati wa upandaji miti aina ya mitende, kazi ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais, Philip Mpango Machi 18, mwaka huu.

Alisema ni jambo la kushangaza na lenye aibu kuona miti iliyopandwa na serikali karibu na makazi ya wananchi inakosa afya na kukauka.

"Ni aibu watu wamekuja kukupandia mti nyumbani kwako wewe unashindwa hata kumwagilia maji walau wiki Moja," alisema Machali.

Vile vile, alisema miti inayopandwa kwenye mazingira yanayokaliwa na wananchi lazima imwagiliwe maji kama ishara ya kukubali kuitunza.

Machali alisema mji wa Bukoba unahitaji kupendeza na kuvutia ili wageni waende kutembelea mandhari safi kwa kuwa tayari wazawa walishaanza kuweka mipango yao.

"Hii miti inatokana na wazawa wa mkoa huu, ambao ni Watanzania wenzetu wanaoishi ndani na nje ya nchi wakiongozwa na Justine Kimodoi kama mwanzilishi wa kampeni," alisema Machali.

Ofisa mazingira katika Manispaa ya Bukoba, Joseph Tambuko, alisema mitende ina faida katika kutunza mazingira na kuepusha mmomonyoko wa ardhi.

"Hii miti aina ya mitende ni rafiki wa mazingira ikizingatiwa Bukoba kuwa na mvua za mara kwa mara, lakini kubwa ni kwamba ikishapandwa na kukua inatumiwa kama vivutio," alisema Tambuko.

# Mpango kuzindua mbio za Mwenge Njombe leo

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, leo anatarajiwa kuzindua mbio za Mwenge wa Uhuru mkoani hapa zitakazofikia kilele chake Oktoba 14, mkoani Kagera.

Akizungumza jana mkoani hapa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, alisema kuwa baada ya uzinduzi wa mbio hizo, vijana sita walioandaliwa kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, watakimbiza katika mikoa 31 na halmashauri 195 nchini kwa siku 195.

"Mwenge wa Uhuru utafanya kazi ya kuhamasisha amani, umoja, upendo na mshikamano wa kitaifa pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki shughuli za maendeleo katika maeneo yao ambapo ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu umezingatia, hoja, na vipaumbele vya serikali ikiwa ni pamoja na umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 na kaulimbiu ya Mwenge mwaka huu ni 'Sensa ni Msingi wa Mipango ya Maendeleo: Shiriki kuhesabiwa, tuyafikie Maendeleo ya Taifa'.

Alisema matarajio ya serikali ni kama yalivyokuwa maono ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alisema; "Sisi tumekwisha uwasha Mwenge wa Uhuru na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima mahali palipojaa dharau."

Aidha, Prof. Ndalichako alisema kuwa mbio za Mwenge wa Uhuru zitaendelea kuelimisha na kuihamasisha jamii ya Watanzania kuhusu umuhimu wa uzingatiaji wa lishe bora, mapambano dhidi ya rushwa, ugonjwa wa UKIMWI pamoja na mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na Malaria.

Naye, Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omary alisema kuwa mkoa huo umefikia asilimia 99 ya maandalizi na sasa wameendelea kuwapokea viongozi mbalimbali wakitaifa watakaoshiriki katika sherehe za uzinduzi wa mbio hizo.

Aliongeza kuwa Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika wilaya sita za mkoa huo ambapo miradi ya afya, elimu, maji na barabara itazinduliwa. Vilevile, amewaomba wananchi wote wa Njombe na Watanzania kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi katika katika uzinduzi huo.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati.

# Operesheni namba moja-20

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

***DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani.***

***Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati.***

***Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.***

***Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.***




*********************************

"Nimeulizwa swali hilo pale kituoni Magomeni. Nimewaambia mkoba kiukweli haukuwa na pesa kwa sababu hatukuwa na pesa za kuwapa, kwa hiyo tulijaza makaratasi ili waamini kuwa ni kweli, ikiwa tumeweka mtego wa polisi, vinginevyo ingekua balaa."

"Kwa hiyo unazo hizo pesa?"

"Ninazo, tena humu humu ndani, utaziona tu baadaye."

"Huyo mjinga Chala aliyetoa hizo pesa, yeye hajajishughulisha na chochote?

"Labda tukutane naye, halafu umuulize mwenyewe, maana nikisema mimi unaweza kusema najifagilia kwa sababu yeye anakutaka na mimi nakupenda."

"Hivi alidhani pesa ndiyo kila kitu? Ona yeye ametoa pesa halafu amekaa. Na pesa zenyewe hazitoshi, lakini wewe hukuwa na pesa, lakini umefanya maarifa mengi hadi mimi leo hii nimekuwa hai na niko hapa." Diana aliongea kwa hisia kali.

"Yaani afadhali hata marehemu afande Marco, yeye hakutoa pesa, lakini alijitolea kukusaidia kwa kuwatumia askari polisi wenzake."

"Ni kweli Jan, lakini Marco naye alikuwa anafanya hivyo kwa sababu yeye hiyo pia ni kazi yake. Alikuwa anafanya kitu ambacho kiko kwenye uwezo wake wa kikazi. Ila ni wewe peke yako uliyeonekana umeacha kila kitu na kuamua kwenda na mimi." Diana hakumaliza maneno hayo akaanza kulia tena. Safari hii hakulia machozi ya furaha na uchungu. Alilia ya uchungu. Alilia kwa sauti na kwikwi. Jan alimuacha alie. Kuna mtu aliwahi kumwambia mwanamke akilia kwanza muache. Kwa sababu machozi humaliza sumu ya uchungu wote uliomo mwilini. Wanawake wengi wakipatwa na matatizo, uchungu au kuudhiwa hulia. Na wakimaliza wanamaliza kila kitu. Lakini wanaume wao huona aibu kulia, hasa mbele za watu au hata sirini. Huweka maumivu yao vifuani na mioyoni mwao. Sumu haiondoki, wanaendelea kuugulia miaka ya miaka. Ndiyo maana huwa ni wagumu wa kusamehe kuliko wanawake. Mara nyingi huwafanya kutangulia kufa kuliko wanawake.

****************************

"Ina maana mwanaume wewe, hizo milioni zako kumi na tano ndiyo ukaona tayari umemaliza? Tatizo halikuwa pesa, tatizo ulikuwa ni uhai wangu." Diana alisema kwa sauti kali.

"Najua, ila mimi nilipata safari ya ghafla kwenda Nairobi, sikuwepo hapa nchini mpenzi wangu."

"Mpenzi wako nani, nipishe huko, ungekuwa na mpenzi, usingeenda huko ulikokwenda wakati nimetekwa, una raha gani wewe?" Yalikuwa ni maneno ya Diana, akimpasha Challa.

Alikuwa amefika nyumbani kwa mjomba Ken baada ya kusikia Diana amepatikana, baada ya Jeshi la Polisi kuwaua na kuwakamata watekaji.

Hakumkuta mjomba Ken nyumbani hapo, lakini alimkuta Jan, ambaye kwake Challa alimchukuliwa pia ni mjomba wa Diana kama alivyotambulishwa huko siku nyingi zilizopita.

Hata hivyo ukaaji wao ulimshangaza Challa. Aliuona ni kama watu ambao wana uhusiano usio wa kawaida. Hata hivyo na wao hawakujionyesha uhalisia sana, baada ya kusikia anagonga kwenye geti. Wakakaa vizuri. Lakini walikuwa pamoja. Angewakuta vile walivyokuwa mwanzo, naona angezirai.

Pamoja na hayo Challa hakutaka kuhoji chochote. Angeambiwa mambo ya ndugu unahoji kama nani.

Akakutana na Diana ambaye si yule anayemfahamu kabla hajatekwa. Huyu alikuwa amebadilika. Si kwa sura wala rangi, ila mtazamo.

"Basi kama kuna sehemu ambayo nimekukosea mpenzi wangu, naomba tu unisamehe."

"Nimeshakusamehe zamani tu. Ila ujue mimi na wewe tena basi. Nimeamua kuanza maisha mengine na si yale tena?" Akamjibu huku akimtazama kwa namna ambayo Challa hakuipenda.

"Kwani mpenzi umekumbwa na nini, mbona umebadika hivi, ni hayo hayo tu au kuna mengine?"

"Babu eee, siyo kila muda nirudierudie kama matangazo ya vifo. Nimesema hiviii. Mimi sina tatizo na wewe, ila kuanzia leo, wewe na mimi tena basi, na hilo neno kuniita mpenzi wako, ondoa."

"Sikia Diana." Challa alianza kuongea kwa ukali kidogo, lakini ambao haukuwa dhahiri.

"Ukumbuke mimi ndiyo nimetoa milioni kumi na tano zilizosafanya watekaji wawekewe mtego na wakanaswa, sasa kweli sina mchango wowote kwenye hili?"

Diana akacheka kicheko cha dharau cha kike.

"Ulikuwa unasikiliza vyombo vya habari wewe, wale watekaji walikuwa wanataka kiasi gani?"

"Najua milioni hamsini, lakini..."

> **Sina mwanaume, ila tu sitaki kuwa na wewe, mwanaume usiyejua kupenda. Watu wananihangaikia usiku na mchana, wewe unastarehe tu huko na wanawake wengine.**

"Ishia hapo hapo" Alidakia "Kwenye milioni hamsini, ukitoa milioni kumi na tano, inabaki milioni ngapi?" Challa hakujibu. Alibaki akimkodolea macho Diana kwa mshangao.

"Unadhani hizo milioni thelathini na tano, nani amezitoa?"

"Huyo aliyetoa hizo ndiye uliyeamua kumpenda?"

"Nimekwambia pesa siyo kila kitu kwenye maisha, wewe umetoa pesa, lakini kuna wenzio wamehatarisha maisha yao, wamekwenda mstari wa mbele kupambana na wauaji."

Challa, alitabasamu. Tabasamu ambalo si halisi. Lilikuwa ni la maumivu na hasira ndani yake.

"Ninachojua waliopambana ni askari polisi na si raia wa kawaida." Alijibu.

"Ndiyo, aliyepeleka kikosi kupambana nao ni mpenzi wangu, afande Marco. Yeye alijitolea kwenda kufa kwa ajili yangu, siyo wewe. Ila tu kwa bahati mbaya amekufa kwenye mapambano. Amekufa kishujaa." Diana alimjibu Challa.

"Sasa huyo si ameshakufa, nimebaki mimi." Diana akacheka kicheko cha dharau.

"Unasikia Diana, mimi naondoka hapa, na sijakuelewa, ila kama nikigundua kuna mtu amechukua nafasai yangu, basi kichwa chake halali yangu. Sitokubali uangukie mikononi mwa mjinga yoyote yule.

Kwa mbali miguu ilianza kumchezacheza Jan. Alikuwa amekaa kwenye kochi kwa muda mrefu bila kuongea, wala kuingilia maongezi hayo.

Wakati anafunguliwa geti na kuingia, Diana alimwambia Jan asiongee chochote kile na yeye atamaliza kila kitu.

Kama kuna kitu alitaka kuongea, lakini akasita.

"Utaua wangapi ndugu yangu?"

"Ina maana Diana una wanaume wengi kiasi kwamba unaniambia utaua wangapi?"

"Sina mwanaume, ila tu sitaki kuwa na wewe, mwanaume usiyejua kupenda. Watu wananihangaikia usiku na mchana, wewe unastarehe tu huko na wanawake wengine. Mwenyewe unaona umenidanganya kusema ulisafiri, mimi habari zako zote ziko hapa." Diana alisema huku mkono wake wa kulia ukipiga mkono wa kushoto.

Baada ya maneno ya kuudhi, kejeri na dharau kuzidi, Challa akaamua ni bora tu aonndoke.

"Mimi naondoka. Lakini kuondoka kwangu siyo kama yameisha. Ni lazima nione mwisho wake. Muda mfupi huu umetoka lakini umekuwa na jeuri na kiburi. Nina uwezo na pesa za kupeleleza kujua nani anakupa kiburi chote hiki. Na mimi nitadili naye."

"Dili na mimi kwanza, muone vile, hebu ondoka kwetu, na hapa iwe mwanzo na mwisho kukanyaga."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MTIBWA YAJIFUA MCHANA IKIWASUBIRI KAGERA KESHO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, amelazimika kubadili muda wa mazoezi kwa wachezaji wake kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar, itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Mechi kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Kagera Sugar itachezwa kuanzia saa 8:00 mchana.

Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru alisema wachezaji wa timu hiyo sasa wanafanya mazoezi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni ili kujiweka imara kuelekea 'dabi' hiyo ya watengeneza sukari.

"Mechi hiyo itachezwa saa 8:00 mchana, ndiyo maana kocha wetu, Salum Mayanga, amekuwa wakiwafanyisha mazoezi wachezaji mchana wa jua kali ili kuzoea mazingira na majira ya mechi hiyo. Itakuwa mechi nzuri na ngumu, kwani ni 'dabi' ya walima miwa na watengeneza sukari," alisema Kifaru.

Kiongozi huyo alisema anaamini timu yao itafanya vyema katika mechi hiyo kwa sababu tangu kuanza kwa mzunguko wa pili wamekuwa na mwenendo mzuri tofauti na hali ilivyokuwa wakati wa mzunguko wa kwanza.

"Tumecheza mechi tatu, tumeshinda mbili na kutoa sare moja, hivyo inaonyesha kuwa tumeimarika, na mechi hii tunataka tushinde ili tutoke kwenye eneo la hatari," alisema Kifaru.

Aliongeza wamejiandaa kukutana na upinzani katika mechi hiyo kwa sababu kila timu inahitaji kukamilisha hesabu zake mapema na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea kwenye msimu huu.

"Tunataka kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ninaamini tutaendelea kupata pointi kwenye uwanja wetu wa nyumbani, ingawa haitakuwa mechi nyepesi, tunajuana vyema tunapokutana na wenzetu wa Kagera Sugar," Kifaru alisema.

Mtibwa Sugar ina pointi 19 na katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko kwenye nafasi ya 14, imecheza mechi 18, ikishinda michezo minne, sare saba na kupoteza michezi saba.

Yanga yenye pointi 48 ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 wakati Simba iliyoko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi 37 mkononi ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo.



Wachezaji wa Namungo kutoka mkoani Lindi wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Jukwaa la Mitindo lanukia

**Na Saada Akida**

MBUNIFU wa mavazi nchini, Ezra Emmanuel anatarajia kuandaa tamasha maalumu litakalojulikana kama Jukwaa la Mitindo kwa vijana ambalo litafanyika baada ya kumalizika kwa mwezi wa Ramadhani, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana ,Ezra alisema lengo la tamasha hilo ni kukuza vipaji kwa vijana ambao wana ndoto za kuwa wabunifu wa kimataifa.

Ezra alisema tamasha hilo litahusisha wabunifu wachanga na wakongwe kwa ajili ya kuonyesha mavazi yao ya suti pamoja na kuwapa ujuzi wa kushona wabunifu wapya wanaochipukia.

"Tamasha hilo la mitindo litafanyika baada ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani kumalizika, nitakuwa na darasa la kutoa mafunzo ya kushona nguo mbalimbali kwa vijana wenye ndoto za kuwa wabunifu," alisema Ezra.

Aliongeza wabunifu wenye nia ya kushiriki watapaswa kuchangia fedha kidogo katika mafunzo hayo kwa ajili ya kununua baadhi ya malighafi zinazohitajika kwenye tamasha hilo ambalo hutumika kama darasa.

"Rai yangu kwa vijana kujitokeza kwa wingi katika darasa hili ili kuja kupata wakina Ezra wengine katika fani ya mitindo nchini," alisema Ezra.

Aliongeza katika kipindi chote cha miaka 15 amewashonea nguo watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali na kusaidia kupata mialiko nje ya nchi ikiwamo Kenya kwa ajili ya kuwatengenezea mavazi waliohitaji.

## Kipanga yatinga nusu fainali FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la ZFF baada ya kuwafunga ndugu zao KVZ penalti 6-5 katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Amaan juzi usiku.

Kipanga inaungana na Mafunzo, Zimamoto ambazo zinashiriki Ligi Kuu Zanzibar kutinga hatua hiyo ya nusu fainali huku klabu nyingine ikiwa ni New King kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Bakari 'Cheupe' alisema ratiba ya mechi za hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo itapangwa baada ya klabu zilizotinga hatua hiyo kukutana.

Cheupe alisema Kamati ya Mashindano inatarajia kukutana na timu hizo kesho ili kujadiliana kwa pamoja juu ya kucheza hatua hiyo.

Alisema uamuzi wa kukutana na timu hizo unatokana na kuingia Mwezi wa Ramadhani, hivyo lazima wakubaliane muda wa kucheza kama iwe ndani ya mwezi huo au baadaye.

Bingwa wa michuano hiyo ya Kombe la FA atapata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## BMZ yawanoa viongozi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BARAZA la Michezo Zanzibar (BMZ), limeendesha mafunzo ya uongozi na utafutaji masomo kwa vyama vya michezo visiwani hapa kwa ajili ya kuvijengea uwezo vyama hivyo kutafuta wadhamini wa ligi mbalimbali wanazoshiriki.

Mafunzo hayo yalikuwa ya siku tatu na yalifanyika kwenye ukumbi wa mchezo wa meza ulioko katika Uwanja wa Mau na kuhudhuriwa na viongozi wa vyama mbalimbali ambavyo vimesajiliwa.

Akizungumza katika hafla ya ufungaji wa mafunzo hayo, Katibu wa BMZ, Said Kassim Marin, alisema lengo kuu la kuandaa toa mafunzo hayo ni kuwaelimisha viongozi wa vyama vya michezo namna ya kupanga safu ya uongozi kwenye vyama vyao lakini pia kujitafutia wadhamini wao wenyewe.

Alisema changamoto kubwa iliyopo katika vyama vingi ni kukosa vitengo vya Idara ya Habari na Masoko ambao wao ndio wenye uwezo wa kutafuta fedha kutoka kwa makampuni na taasisi mbalimbali.

Aliongeza anaimani mafunzo hayo yatavisaidia vyama hivyo vya michezo kubadili na kufanya mambo yao kisasa ikiwamo kutafuta udhamini wa kuendesha shughuli zao za kila siku huku akimtaja Mkufunzi alikuwa ni Suleiman Mahmoud Jabir.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA KUIBOMOA CHELSEA

BARCELONA imepeleka dau ili kutumia faida ya vikwazo ilivyowekewa Chelsea kwa kujaribu kuwasajili mabeki wake watatu waliowahi kushinda kombe la ligi ya mabingwa Ulaya, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29, Cesar Azpilicueta (32) na Andreas Christensen (25). (***Telegraph***)

### RONALDO KUONDOKA UNITED

KLABU ya Manchester United inatarajia mshambuliaji wake, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu, akiwa ametumia nusu tu ya miaka miwili ya mkataba wake. (***Football Insider)***

### TIELEMANS BADO YUPO

LEICESTER City ina matumaini ya kumshawishi kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24 kusaini mkataba mpya, licha ya kusakwa na klabu za Manchester United Arsenal. (***Team Talk)***

### VILLA KUMWACHA LUIZ

KIUNGO wa Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 23 anaweza kuondoka Aston Villa msimu huu, huku kocha wa timu hiyo, Steven Gerrard akiipa kipaumbele kikubwa nafasi ya kiungo mkabaji kwenye usajili wa msimu ujao. (***Mail***)

### VESTERGAARD MAMBO SAFI

KLABU ya Everton inajiandaa kumsajili mlinzi wa kati wa Leicester City kutoka Denmark, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 29. (Football Insider)

### SPENCE AWEKWA SOKONI

MLINZI wa Middlesbrough, Djed Spence anayecheza kwa mkopo Nottingham Forest, anataka kuhamia Ligi Kuu England huku Arsenal na Tottenham zikuhusishwa na uhamisho wake wa gharama ya pauni milioni 20 mwishoni mwa msimu. Manchester United pia inamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa England chini ya miaka 21. (***Mirror***)

### LEEDS YAMTAKA DEST

KLABU ya Leeds United inamtaka mlinzi wa pembeni wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21. (***Team Talk***)

### GARNER SASA KIMEELEWEKA

KLABU ya Nottingham Forest inataka kubadili mkopo wa kiungo, James Garner mwenye umri wa miaka 21 kutoka Manchester United kuwa usajili wa kudumu mwishoni mwa msimu, lakini hilo litategemea kama watafanikiwa kupanda daraja kucheza Ligi Kuu England. (***Football Transfers***)

### NKUNKU AGEUKA LULU

RB Leipzig wanajiandaa kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo Mfaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24 msimu huu. Manchester United, Liverpool, Paris St-Germain, Real Madrid, Manchester City, Arsenal na Bayern Munich zote zinamfuatilia. (***ESPN***)

### MCNALLY ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham imepeleka dau la pauni milioni mbili kwa ajili ya mlinzi wa kati wa Oxford United, Luke McNally mwenye umri wa miaka 22. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AJIPANGA KUIPAISHA ARSENAL

●●● Ahitaji kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya...

**LONDON,** ENGLAND

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta bado hazifikirii timu nyingine katika kinyang'anyiro cha kuwania nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu England, akisisitiza yote yamo mikononi mwa Washikabunduki hao.

Kikosi cha Arteta kimepoteza mchezo mmoja tu kati ya nane ya Ligi Kuu England tangu kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Manchester City mwanzoni mwa 2022, na hivyo kupanda jedwali hadi nafasi ya nne kwenye ligi hiyo.

Arsenal wamo pointi tatu mbele ya Tottenham walio katika nafasi ya tano, ambao wamecheza mechi moja zaidi, huku wakipigania kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku mechi yao ijayo ni ya ugenini dhidi ya Crystal Palace na itachezwa keshokutwa.

Hiyo ina maana Spurs, Manchester United na West Ham watakuwa wamecheza kabla ya Arsenal kushuka katika dimba la Selhurst Park, lakini Arteta haoni kuchelewa kwa mchezo wao kama faida zaidi ya washindani wake.

"Tutazingatia kile tunachoweza kufanya. Hilo ndilo jambo pekee tunaloweza kudhibiti," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Kupitia TV tunaweza kuteseka na tunaweza kufurahia na hakuna mengi zaidi tunaweza kufanya. Tunachopaswa kufanya ni kushinda mechi za soka ambazo tunahitaji kufikia kile tunachotaka na hiyo yote iko mikononi mwetu."

Aaron Ramsdale alikosa ushindi wa 1-0 dhidi ya Aston Villa mara ya mwisho, huku Bukayo Saka akifunga goli la ushindi kabla ya kuugua na kushindwa kwenda kwenye majukumu ya Timu ya Taifa.

Arteta alithibitisha Saka amerejea mazoezini.

"Bukayo anajisikia vizuri," aliongeza. "Anafanya mazoezi leo (jana), kwa matumaini ikiwa bado anajisikia kama alivyokuwa jana (juzi). Aaron bado anajisikia vibaya, bado hajafanya mazoezi kwa hivyo hatujui kama atakuwapo kwenye mchezo wa Jumatatu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,089

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
LEICESTER
1 | 1.56
X | 4.26
2 | 5.10

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# COURTOIS AFURAHIA KURUDI CHELSEA



**MADRID,** Hispania

NYOTA Thibaut Courtois anafurahia kile anachotarajia kitakuwa "maalum" kurejea Stamford Bridge wakati Real Madrid watakapomenyana na Chelsea katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Madrid waliwatoa Paris Saint-Germain katika hatua ya 16 bora, huku The Blues wakiwaondoa mabingwa watetezi wa Ligue 1, Lille kwa mabao 4-1.

Timu hizo zilipangwa pamoja katika hatua ya nane bora katika marudio ya nusu-fainali ya mwaka jana, ambayo Chelsea ilishinda mabao 3-1 na kunyanyua taji hilo. Courtois alicheza katika mechi zote mbili, pamoja na sare ya nyumbani iliyochezwa kwenye Uwanja wa Alfredo Di Stefano.

Mashabiki wa Blues hawakufurahishwa na jinsi Courtois alivyoondoka, lakini kipa huyo anaangazia zaidi mataji mawili ya Ligi Kuu na makombe mawili ya nyumbani aliyoshinda akiwa na klabu hiyo.

Iwapo watapitia, Chelsea itakuwa timu ya kwanza ya England kuwaondoa Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa mara kadhaa. Los Blancos wamekutana na Chelsea mara nyingi bila kushinda kuliko walivyocheza na timu nyingine yoyote kwenye mashindano ya Ulaya, sare mara mbili na kupoteza mara tatu.



# *Busquets ana ndoto Mess[i] kurejea Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Sergio Busquets atamrudishia kitambaa cha unahodha Lionel Messi ikiwa fowadi huyo atarejea Camp Nou.

Nahodha wa Timu ya Taifa ya Argentina, Messi aliondoka Blaugrana kwa uhamisho wa bure na kujiunga na Paris Saint-Germain Agosti, mwaka jana huku Barca iliyokuwa na matatizo ya kifedha ikishindwa kutimiza masharti ya mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 bado hajawa kwenye kiwango chake kwenye Ligue 1, akifunga mabao saba pekee katika mashindano yote akiwa na kikosi hicho cha Kocha, Mauricio Pochettino.

Kumekuwa na uvumi gwiji huyo anaweza kuondoka PSG - ambao wanaweza pia kumpoteza, Kylian Mbap
anayetarajiwa kwen
Real Madrid - mwish
mwa msimu huu, na 
cha mkuu wa Barca, X
alipendekeza mlan
utakuwa wazi kila wak
kwa kurejea kwa Mess

Mchezaji mwenza
wa zamani Busqu
aliunga mkono maoni
Xavi alipokuwa akielez
hamu yake ya mshin
huyo mara saba wa B
lon d'Or kurejea Hisp
ia.

9,062,840

# COASTAL UNION YAMREJESHA MGUNDA KUMALIZIA MSIMU

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Coastal Union ya jijini Tanga umeamua kumrudisha kocha wake wa zamani, Juma Mgunda kukiongoza kikosi kikosi cha timu hiyo hadi mwishoni mwa msimu huu, imefahamika.

**Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Coastal Union jana ilisema Mgunda, straika wa zamani wa timu hiyo amechukua nafasi iliyoachwa wazi wa aliyekuwa Kocha Mkuu, Melis Medo ambaye aliondolewa klabuni hapo.**

"Uongozi wa Coastal Union unapenda kuujulisha umma kuwa umembadilishia majukumu Mkurugenzi wa Ufundi, Juma Mgunda, na sasa atakuwa Kocha Mkuu ambaye atakinoa kikosi hicho hadi mwishoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliongeza tayari Mgunda ameanza kazi ya kukinoa kikosi hicho na atasaidiana na Joseph Lazaro.

Mgunda ambaye ameanza kazi ya kukinoa kikosi hicho juzi, aliondolewa katika nafasi hiyo Agosti, mwaka na kupewa kazi ya Ukurugenzi wa Ufundi, na nafasi yake ilichukuliwa na kocha Medo, raia wa Marekani lakini ameshindwa kumudu kwa muda mrefu.

Kutokana na mabadiliko hayo, Lazaro, beki wa zamani wa Coastal Union, ambaye alikuwa akikaimu nafasi ya Kocha Mkuu, anarejea katika nafasi yake ya awali ya Kocha Msaidizi.

Naye Mgunda amewataka mashabiki wa timu hiyo kumpa ushirikiano ili wafikie malengo yao ya kujiimarisha katika msimamo wa ligi.

Mgunda alisema ameamua kurudi katika nafasi hiyo kutokana na mapenzi makubwa aliyonayo na klabu yake hiyo. Hata hivyo alisema ataendelea kuishikilia nafasi hiyo mpaka hapo atakapopatikana kocha mkuu mpya.

Coastal Union inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuikaribisha Simba Aprili 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.





Klabu ya Yanga kwa kushirikiana na Kampuni ya GSM Foundation wakiwa katika picha ya pamoja na wawakilishi wa vituo vya watoto yatima ambavyo vimepata msaada wa chakula kwa ajili ya kuupokea mwezi wa Ramadhani. **PICHA: YANGA SC**

# *Pan African, DTB FC hapatoshi*

**Na Shufaa Lyimo**

KAIMU Kocha Mkuu wa Pan African, Ahmed Waziri, amesema kikosi chake kiko kamili kuwakabili DTB FC katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Waziri alisema maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na wachezaji wao wote wako tayari kuwakabili vinara hao wa Ligi Daraja la Kwanza.

"Tunafahamu tunakwenda kukutana na timu ambayo inaongoza katika ligi, hivyo tutaingia tukiwa na tahadhari kubwa," alisema Waziri.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wana morali ya hali ya juu na wameahidi watapambana kuhakikisha wanapata pointi zote tatu.

Alisema lengo ni kufanya vizuri na kupanda nafasi ya juu na kudai makosa yaliyojitokeza katika michezo iliyopita wanaendelea kuyafanyia kazi.

"Tutapambana kuhakikisha malengo yetu yanatimia, tunawaheshimu wapinzani wetu, tunajua hautakuwa mchezo rahisi,' Waziri alisema.

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/04/22 | 17:00 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.53 | 2.83 |
| 02. 02/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 03. 02/04/22 | 19:30 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.38 | 3.59 | 2.69 |
| 04. 03/04/22 | 14:00 | Rangers vs Celtic | 2.36 | 3.28 | 2.88 |
| 05. 03/04/22 | 15:30 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 06. 03/04/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 07. 03/04/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 08. 03/04/22 | 16:00 | Atalanta vs Napoli | 2.42 | 3.20 | 2.90 |
| 09. 03/04/22 | 16:30 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.86 | 3.26 | 2.45 |
| 10. 03/04/22 | 19:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.59 | 3.03 | 2.79 |
| 11. 03/04/22 | 19:30 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.13 | 2.73 |
| 12. 03/04/22 | 20:00 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.80 | 3.20 | 2.47 |
| 13. 03/04/22 | 21:45 | Juventus vs Inter | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 02/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5287 | Liverpool vs Watford | 1.13 | 8.17 | 16.93 |
| 15:00 | 1679 | Partizan vs Backa Topola | 1.17 | 6.20 | 11.63 |
| 15:00 | 3749 | Getafe vs Mallorca | 2.15 | 2.98 | 3.84 |
| 16:00 | 1801 | Spezia vs Venezia | 2.08 | 3.29 | 3.49 |
| 16:00 | 3291 | Mbeya City vs Geita Gold FC | 1.90 | 2.98 | 4.20 |
| 16:00 | 4500 | Kayserispor vs Fenerbahce | 3.58 | 3.58 | 1.94 |
| 16:30 | 1846 | Arminia Bielefeld vs Stuttgart | 2.99 | 3.29 | 2.31 |
| 16:30 | 2126 | Eintracht Frankfurt vs Greuther Furth | 1.46 | 4.62 | 6.02 |
| 16:30 | 2211 | SC Freiburg vs Bayern Munchen | 5.21 | 4.71 | 1.50 |
| 16:30 | 3602 | Hoffenheim vs VfL Bochum | 1.50 | 4.49 | 5.59 |
| 16:30 | 4910 | Bayer Leverkusen vs Hertha BSC | 1.42 | 4.92 | 6.23 |
| 17:00 | 1288 | St Johnstone vs Livingston | 2.65 | 2.84 | 2.89 |
| 17:00 | 1850 | Brighton vs Norwich City | 1.49 | 4.09 | 6.58 |
| 17:00 | 3333 | Burnley vs Manchester City | 10.84 | 5.42 | 1.26 |
| 17:00 | 3470 | Dundee FC vs Aberdeen | 3.79 | 3.10 | 2.05 |
| 17:00 | 3783 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.89 | 3.04 | 2.54 |
| 17:00 | 4071 | Motherwell vs St Mirren | 2.21 | 3.10 | 3.35 |
| 17:00 | 4164 | Hibernian vs Dundee Utd | 1.80 | 3.38 | 4.47 |
| 17:00 | 4433 | Chelsea vs Brentford | 1.34 | 4.79 | 8.79 |
| 17:00 | 4634 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.55 | 2.75 |
| 17:00 | 4891 | Ross County vs Hearts | 3.87 | 3.33 | 1.94 |
| 17:15 | 1011 | Levante vs Villarreal | 3.58 | 3.68 | 1.97 |
| 17:15 | 5192 | Zulte Waregem vs St Truiden | 2.79 | 3.38 | 2.38 |
| 17:30 | 3165 | Groningen vs Ajax | 10.85 | 6.12 | 1.21 |
| 18:00 | 5872 | Nice vs Rennes | 3.02 | 3.32 | 2.31 |
| 19:00 | 1533 | Molde vs Valerenga | 1.53 | 4.38 | 5.17 |
| 19:00 | 4413 | Lazio vs Sassuolo | 1.72 | 4.10 | 4.10 |
| 19:30 | 3467 | Mechelen vs Kortrijk | 1.66 | 3.99 | 4.48 |
| 19:30 | 3587 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.36 | 3.64 | 2.69 |
| 19:30 | 4036 | Celta Vigo vs Real Madrid | 3.74 | 3.50 | 1.97 |
| 19:30 | 4142 | Manchester Utd vs Leicester | 1.56 | 4.26 | 5.10 |
| 19:30 | 4773 | Oostende vs RFC Seraing | 2.18 | 3.43 | 3.08 |
| 19:45 | 4118 | Twente vs PSV Eindhoven | 4.36 | 3.61 | 1.74 |
| 20:00 | 3436 | Lille vs Bordeaux | 1.49 | 4.34 | 6.06 |
| 20:00 | 4630 | GD Estoril vs FC Vizela | 2.30 | 3.28 | 2.98 |
| 20:00 | 4946 | Sparta Prague vs Banik Ostrava | 1.53 | 4.35 | 5.67 |
| 20:30 | 3457 | Galatasaray vs Fatih Karagumruk | 1.70 | 3.78 | 4.48 |
| 21:00 | 1195 | Legia Warszawa vs Lechia Gdansk | 1.94 | 3.22 | 3.66 |
| 21:00 | 1283 | AZ Alkmaar vs Vitesse Arnhem | 1.62 | 3.83 | 4.97 |
| 21:00 | 5794 | Waalwick vs Utrecht | 3.82 | 3.52 | 1.87 |
| 21:30 | 1541 | FC Sion vs St. Gallen | 3.15 | 3.50 | 2.12 |
| 21:45 | 5298 | Salernitana vs Torino | 4.00 | 3.45 | 1.89 |
| 21:45 | 5874 | OH Leuven vs Royal Antwerp | 3.33 | 3.62 | 2.01 |
| 22:00 | 1990 | Atletico Madrid vs Alaves | 1.38 | 4.64 | 8.27 |
| 22:00 | 2550 | Feyenoord vs Willem II Tilburg | 1.14 | 7.34 | 14.88 |
| 22:00 | 3832 | St Etienne vs Marseille | 3.47 | 3.32 | 2.10 |
| 22:30 | 2629 | Famalicao vs Boavista | 2.06 | 3.22 | 3.57 |
| 22:30 | 4325 | Chicago Fire vs FC Dallas | 2.01 | 3.39 | 3.74 |
| 23:00 | 1341 | Toronto FC vs New York City | 3.43 | 3.53 | 2.06 |
| 23:00 | 4281 | FC Cincinnati vs Montreal Impact | 2.40 | 3.47 | 2.82 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumamosi Aprili 2, 2022
Nipashe



Courtois afurahia kurudi Chelsea UKURASA 22

TUUJAZE UWANJA...



Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally (aliyeshika kipaza sauti), akiwasisitiza mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuishangilia timu yao katika mchezo wake wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendermerie utakaochezwa kesho usiku. **PICHA: SIMBA SC**

# YANGA YATANGAZA MAPAMBANO BARA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## Kaze afunguka wameingia katika wiki nane ngumu lakini tayari...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze amesema kikosi chake kinaingia katika miezi miwili migumu lakini wamejipanga kupambana kuhakikisha wanafikia malengo ya kushinda mechi zote ili kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, Tanzania Bara na Kombe la FA msimu huu.

**Kaze alisema timu yao itakuwa na ratiba ngumu kwa mwezi huu na ujao na hiyo ndio fainali yao na kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika michezo yote wakianzia mechi dhidi ya Azam FC itakayochezwa Jumatano ijayo.**

Kocha huyo alisema mara kadhaa amekuwa akiwasisitiza wachezaji kuongeza umakini na kujifunza mbinu mpya ili kuhakikisha wanafanikiwa katika malengo waliyonayo ya kushinda michezo yote iliyoko mbele yao.

"Hii miezi miwili ya fainali kwetu kwa sababu tunahitaji kupambana kushinda mechi zote zilizopo mbele yetu, tunacheza na Azam FC halafu mechi ya FA (dhidi ya Geita), kabla ya Simba hizo zote ni mechi za muhimu kwenye makombe mawili tofauti," alisema Kaze.

Alisema kiufundi mechi chache lakini ni ngumu na zilizo muhimu kupata matokeo chanya wakati msimu ukielekea tamati.

"Mei ni mwezi wa kumalizia kila kitu, sasa unaweza kuona jinsi ratiba ilivyo na umuhimu, tunahitaji kufanya mazoezi ya pamoja kwa muda mrefu na kupata mechi za kirafiki, kujiweka sawa katika kufikia malengo yetu," alisema Kaze.

Aliongeza mchezo dhidi ya Azam FC ni mechi muhimu na inayotarajiwa kuwa na ushindani mkubwa lakini dhamira yao ni kuhakikisha wanapata pointi tatu.

Mrundi huyo pia alisema tayari ameanza kutengeneza mfumo mwingine wa uchezaji ambao utawasaidia wakikutana na mechi ngumu, au kwenye viwanja vya mikoani ambavyo si rafiki.

"Tumejipanga kuhakikisha timu inakuwa na mifumo mbalimbali ya uchezaji na si kutegemea mfumo mmoja ambao siku ukitakaa, au ukikuta uwanja hauruhusu, au wapinzani kukudhibiti, basi timu inakosa njia nyingine ya kufanya," alisema Kaze.

Mrundi huyo aliongeza katika mechi ya kirafiki dhidi ya Mafunzo iliyochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, kuna wakati alichezesha mastraika wawili mbele, Fiston Mayele na Heritier Makambo, wakiwa na mfumo wa 4-4-2, lengo ikiwa ni kutazama mfumo mwingine, hasa pacha ya wachezaji hao wawili mbele, ambao anaamini baadaye unaweza kuwasaidia.

"Tulianza na mfumo tuliozoea, lakini baadaye tukachezesha mastraika wawili mbele, hiyo ni kutaka kujaribu aina nyingine ya mfumo, maana kuna siku tutataka kutumia mastraika wawili, kama siku hiyo mechi itakuwa ngumu, matokeo mazuri hajayapatikana, au kwenye viwanja vigumu, sasa tunaona kama tunaweza kuwatumia Mayele na Makambo wote kwa pamoja ili wakae pale mbele, wawape presha mabeki, mawinga nao wawe wanakwenda pembeni na kupiga krosi nyingi," Kaze alisema.

Yanga yenye pointi 48, ndio timu pekee mpaka sasa haijapoteza mechi yoyote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa inaongoza katika msimamo baada ya kushinda mechi 15 na sare michezo mitatu.

Kikosi cha Yanga kiliingia kambini jana rasmi kuanza maandalizi ya kuwakabili Azam FC.

# Simba mzuka juu

**Na Saada Akida**

WAKATI ikizindua safari ya treni kuelekea mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendermerie, benchi la ufundi limesema wanasubiri muda kukamilisha majukumu waliyonayo ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Simba itaikaribisha US Gendermerie katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi itakayochezwa kesho kuanzia saa 4:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako katika hali nzuri na wameahidi kujituma kwa ajili ya kufikia malengo ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Pablo alisema anafahamu ugumu watakaokutana nao katika mchezo huo lakini anawaondoa hofu mashabiki wa Simba kwa sababu hawatabweteka huku kila mchezaji akitarajia kutimiza ndoto ya kufanya vizuri.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, ameliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na anawasisitiza mashabiki kufika uwanjani kesho ili kuongeza hamasa kwa wachezaji wao.

"Tunapenda pia kuwaambia mashabiki wetu ukienda kununua jezi ya Simba dukani kwa Vunja Bei, utapewa na tiketi ya bure ya Sh. 3,000, hii tumeweka ili kuhakikisha tunaujaza uwanja siku ya Jumapili," Ahmed alisema.

Simba inahitaji ushindi ili kujihakikishia tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >